**Kiongozi cha Ufundishaji na Ujifunzaji Unaomzingatia Mwanafunzi**

*Mbinu 70 za ufundishaji shirikishi za kuwahusisha*

*na kuwahamasisha wanafunzi wa kitanzania*



*Mtoto ni kama mche unaoweza kuwa na ukuaji uliodumaa na kusongwa, au utakaolishwa mpaka ukue kuzidi urefu wa kujitegemea au ambao matawi yake yanaweza kupogolewa na kufunzwa ili matunda mengi yapatikane wakati wa upevu. Na watu wenye fursa ya kuwatengeneza hawa watoto –wenye uwezo huo- ni walimu katika shule zetu.*

-*Julius K. Nyerere*

*Chuo cha Ualimu Morogoro, 1966*

**Kimeandikwa Na**

Ian Keith, Allen Rugambwa, Frances Vavrus na Adrian Maganga

**PROJECT ZAWADI** **JULY 2016**

## UTANGULIZI

Kiongozi cha ufundishaji na ujifunzaji shirikishi ni jitihada za pamoja na Project Zawadi, Zinduka, na timu ya uongozi wa shule za Tanzania, wakuu wa shule na walimu katika wilaya ya Bunda Vijijini, Tanzania. Aidha, Profesa Frances Vavrus wa Chuo Kikuu Cha Minnesota Marekani na Allen Rugambwa wa Chuo Kikuu Cha Kikatoliki cha Mwenge Tanzania walichangia kupanua na kuumba maudhui ya kiongozi hiki kwa kutumia nyenzo zitokanazo na kazi yao ya pamoja kwenye mpango wa '*Teaching in Action*'. Mpango huu unatilia mkazo ufundishaji shirikishi nchini Tanzania.

Project Zawadi (PZ) ni shirika lisilotafuta faida lililoanzishwa Desemba 2000. Linafanya kazi katika mkoa wa mara, Tanzania. Kazi ya shirika hili ni kutoa fursa za elimu kwa mayatima na watoto wa kitanzania wasiojiweza ili waweze kujitegemea na kuwa wananchi wachapakazi kwenye jamii zao. Mwanzilishi na rais wa shirika hili ni Brian Singer, aliyewahi kufanya kazi za kujitolea ili kuwezesha watu kimaisha na kielimu nchini Tanzania kwenye miaka ya tisini (1990s). Project Zawadi inafanya kazi na Zinduka nchini Tanzania.

Zinduka ni shirika lisilo tafuta faida lililoko Nyamuswa,Tanzania. Linatoa huduma mbali mbali mathalan kufadhili wanafunzi kielimu, kujenga madarasa na vifaa vingine vya shule, kuendesha kliniki, kutoa mikopo kwa biashara ndogo ndogo, kuendesha miradi ya mafunzo ya ufundi, na kutoa huduma mbalimbali wilayani Bunda vijijini. Zinduka ilianzishwa mwaka wa 2000, na 2012 ikatambulika kama shirika lisilotafuta faida la kitaifa la mwaka na '*Foundation for Civil Society*'. Mkurugenzi mtendaji wa Zinduka ni Max Madoro, kiongozi wa uraia na siasa kaika kata ya Nyamuswa, Wilaya ya Bunda Vijijini, mkoa wa Mara,Tanzania.

Tenda Teachers ina ratibu kazi zake kwa kushirikiana na kamati ya uongozi inayohusisha viongozi wa asasi na walimu wa kutoka shule zifuatazo:-

1. Adrian Maganga - Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mihingo
2. Esther Amboga - Mwalimu wa Shule ya Sekondari Ikizu
3. Dan Singa - Mwalimu wa Shule ya Msingi Olympus
4. Muse Mwisawa - Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiabakari, na mwenyekiti wa Zinduka
5. Regina Mkama -Mwalimu wa Shule ya Msingi Olympus
6. Moreen Muruga - Mwalimu wa Shule ya Msingi Kambubu
7. Edward Ferdinand - Mwalimu wa Shule ya Sekondari Sazira
8. Stephano Kinduru - Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiabakari
9. Hamis Masenza - Mtaalamu wa Teknolojia , Zinduka
10. Maximmilian Madoro - Mkurugenzi Zinduka

Julai 2015, Ian Keith, mwalimu aliyethibitishwa na bodi ya kitaifa kutoka St. Paul, Minnesota nchini Marekani na anayefanya kazi ya kujitolea kwa hiari na Project Zawadi, aliendesha mafunzo ya walimu na kufundisha nao madarasani, Bunda Vijijini. Mradi wa kiongozi cha ufundishaji shirikishi (*LCT*) ulianzishwa ndani ya kipindi hicho, na uongozi ukawekwa ili kusimamia kazi hiyo.

Julai na Agosti 2016 walimu wa kitanzania kutoka shule nne wilayani Bunda Vijijini na shule tano kutoka mkoa wa Kilimanjaro watachukuliwa video wakionyesha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji

shirikishi (*LCTs*) madarasani mwao. Nakala ya kiongozi hiki inapatikana kwenye tovuti ya Project Zawadi http://projectzawadi.org/programs/tenda-teachers/. Vile vile, video fupi za *LCT* teuliwa na maelezo mengine kuhusu Tenda Teachers Project vinapatikana Facebook kwenye: www.facebook.com/TendaTeachers/. Video zote zinaweza pia kupatikana kwenye tovuti ifuatayo ya You Tube: www.tinyurl.com/tendateachers. Lengo la mradi huu ni kuwapa walimu wa kitanzania na wale walioko mafunzoni maelezo na video za *LCTs* ili kuwasaidia kuboresha fani yao ya ufundishaji.

Kiongozi hiki kimeandikwa kutoka kwa kazi mbali mbali. Kazi hizi zimetambuliwa katika sura ya kwanza, ya pili, na sehemu ya marejeo. Wasifu wa waandishi umeandikwa katika sehemu ifuatayo.

## WASIFU WA WAANDISHI

Kiongozi hiki kimeandikwa na Ian Keith kwa msaada wa Adrian Maganga. Kazi yao ilipanuliwa na kupangiliwa na Allen Rugambwa pamoja na Frances Vavrus kwa kutumia nyenzo walizoziandika kwa ajili ya utaratibu wa *TIA*. Uhakiki tamati wa kiongozi hiki ulifanywa na Profesa Vavrus. Wasifu mfupi wa kila mwandishi kulingana na kitabu hiki na Project Zawadi umeandikwa hapa.

**Ian Keith** ndiye mwandishi mkuu wa kiongozi hiki. Yeye ni mwalimu mkongwe kazini aliyefundisha kwa miaka 30 katika shule ya St. Paul, Minnesota (Marekani). Ni mwalimu aliyethibitishwa na bodi ya kitaifa katika ujuzi wa kusoma na kuandika kwa awali, na amewahi kuwa rais wa shirikisho la walimu wa St.Paul, na ni mjumbe wa bodi ya Project Zawadi. Alikuja nchini Tanzania mnamo Julai 2015 na kufundisha walimu 120 kutoka shule 16 katika wilaya ya Bunda Vijijini kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji shirikishi.

**Frances Vavrus** ni Profesa katika Chuo Kikuu cha Minnesota (Marekani) na ni mwandishi wa kazi mbalimbali zilizochapishwa kuhusu elimu ya kitanzania. Ni mhariri mwenza wa *Teaching in Tension*, kitabu kinachoonyesha jinsi ambavyo walimu wa kitanzania wanatumia mbinu za ufundishaji shirikishi. Pia, ni mwanzilishi mwenza wa *Teaching in Action (TIA)*, mpango unaoshirikisha walimu katika maendeleo ya fani yao katika Chuo Kikuu Cha Kikatoliki cha Mwenge. Profesa Vavrus pia ni mjumbe wa bodi ya Project Zawadi.

**Allen Rugambwa** ni mhadhiri msaidizi katika Chuo Kikuu Cha Kikatoliki cha Mwenge. Anawezesha ufanisi wa *TIA* na utaratibu wa mafunzo ya mashuleni katika shule za sekondari kusini mwa Tanzania. Akishirikiana na Profesa Vavrus na wahadhiri wengine wa Chuo Kikuu Cha Kikatoliki cha Mwenge, ameandika miongozo mingi kuhusu ufundishaji unaomshirikisha mwanafunzi. Miaka ya nyuma aliongoza warsha mbili za mafunzo zilizoendeshwa na Project Zawadi. Vile vile, alishiriki katika uandishi wa *Teaching in Tension.*

**Adrian Maganga** ndiye mwalimu kiongozi na msimamizi wa mradi huu nchini Tanzania. Yeye ni mwalimu wa Kiingereza katika shule ya Sekondari Mihingo, na ni mjumbe wa timu ya uongozi nchini Tanzania.

## YALIYOMO


**UTANGULIZI** ........ **Error! Bookmark not defined.**

**WASIFU WA WAANDISHI** ........ **Error! Bookmark not defined.**

**VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA** ........ **Error! Bookmark not defined.**

**SURA YA KWANZA: Dibaji** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Ufafanuzi wa Istilahi LCT ........ **Error! Bookmark not defined.**

Kanuni za LCT ........ **Error! Bookmark not defined.**

Faida za LCT ........ **Error! Bookmark not defined.**

*LCT* Katika Sera za Serikali ya Tanzania ........ **Error! Bookmark not defined.**

Sifa za Mwalimu Shirikishi kwa Mazingira ya Kitanzania ........ **Error! Bookmark not defined.**

Nadharia Zinazoongoza *LCT* ........ **Error! Bookmark not defined.**

Nadharia ya Utambuzi ........ **Error! Bookmark not defined.**

Nyanja za Utambuzi za Bloom ........ **Error! Bookmark not defined.**

Nadharia ya Akili Nyingi ........ **Error! Bookmark not defined.**

Hitimisho ........ **Error! Bookmark not defined.**

**SURA YA PILI: Kujenga Mazingira Chanya Darasani** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #1 Fundisha kwa Shauku** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu # 2 Jenga kwenye Uchanya** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu # 3 Onyesha Matarajio ya Juu** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #4 Wanafunzi Wote Wanaweza Kujifunza** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #5 Sherehekea ushindi** ........ **Error! Bookmark not defined.**

**SURA YA TATU: Kuandaa Somo Linalomzingatia Mwanafunzi** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #6 Masomo Yenye Hatua Kuu Tano** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #7 Somo la Ugunduzi ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #8 Anza na Mwisho Akilini** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #9 Andika Malengo ya Somo** ........ **Error! Bookmark not defined.**

**SURA YA NNE: Lcts Mwanzoni mwa Somo** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #10 Jedwali la “KWL”** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #11 Tatizo katika Mazingira ya Kawaida** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #12 Simulia Kisa** ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #13 Andika Upesi ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #14 Kanda ya Picha au Sauti ........ **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #15 Barometa ya Jamii ............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #16 Mnyororo wa Majina** .................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #17 Nisahili ................................................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #18 Mchezo wa Kweli Nne (Moja si Kweli) .............................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #19 Kuonyesha Vipaji ............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #20 Duara ya Marafiki ............................................................ **Error! Bookmark not defined.**
**SURA YA TANO: Mbinu za Uulizaji Maswali** ................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #21 Hakuna Mikono** ................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #22 Muito na Muitikio** ............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #23 Uliza Tena** ....................................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #24 Rahisisha Swali** ................................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #25 Nielezee Zaidi** .................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #26 Kubali au Kataa** ............................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #27 Swali la Siku** ..................................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #28 Maswali ya Wote** ............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #29 Uliza Maswali ya Nyanja za Juu za Utambuzi** .................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #30 Maswali ya Upesi ................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #31 Subiri Muda ......................................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #32 Ipate Sawa sawa ................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #33 Maswali Rejeshi .................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
**SURA YA SITA: LCTs za Ujenzi na Uimarishaji wa Maarifa** ....................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #34 Utafiti Maalum** ................................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #35 Kila mtu Anaandika** .......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #36 Sentensi Anzilishi** ............................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #37 Kuta za Maneno** ............................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #38 Vikomo vya Muda** ............................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #39 Mwanzo Mzuri** ................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #40 Mhadhara Shirikishi ............................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #41 Kuonyesha Kazi za Wanafunzi kwa Ujifunzaji ......................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #42 Kutembelea Vituo vya Maonyesho ........................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #43 Mazoezi ya Mmoja Mmoja .................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #44 Imla ....................................................................................... **Error! Bookmark not defined.**

Mbinu #45 Egesho la Maswali ........ Error! Bookmark not defined.
**SURA YA SABA: Kazi Za Wawili Wawili na za Vikundi** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #46 Geuka na Zungumza** ........s**Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #47 Fikiri-Ungana-Shirikishana** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #48 Kazi za Wawili Wawili** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #49 Ufundishaji Rika** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #50 Vikundi vya Mjadala Vinavyoongozwa na Wanafunzi** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #51 Uwasilishaji wa Mada Darasani** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #52 Usomaji wa Awali Unaofuatiwa na Mijadala ya Vikundi ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #53 Maigizo ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #54 Kuwatoa Wanafunzi Nje ya Darasa ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #55 Makundi ya Chemshabongo ........ **Error! Bookmark not defined.**
**SURA YA NANE: Lcts kwa Tathmini Na Hitimisho** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #56 Tiketi ya Kutokea** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #57 Nionyeshe** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #58 Vichwa Chini, Mikono Juu** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #59 Mchezo wa Kurusha Mpira ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #60 Mchezo wa Kofia ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #61 Kipande cha Mfano ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #62 Kiti cha Moto ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #63 Toa Muhtasari ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #64 Kusahihisha kwa Mnyororo ........ **Error! Bookmark not defined.**
**SURA YA TISA: Usimamizi wa Darasa** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #65 Weka Taratibu** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #66 Matokeo – Ya Haki, ya Kueleweka na Thabiti** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #67 Ishara za Kimya** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #68 Kila Mtu Anafanya Hivyo** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #69 Sauti Imara na Msimamo** ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mbinu #70 3/ 5/ 1** ........ **Error! Bookmark not defined.**
**HITIMISHO** ........ **Error! Bookmark not defined.**
**TASNIFU** ........ **Error! Bookmark not defined.**

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

| | |
|---|---|
| **LCT** | Learner-Centered Teaching |
| **LCTs** | Learner-Centered Teaching Techniques |
| **MOEVT** | Ministry of Education and Vocational Training |
| **PZ** | Project Zawadi |
| **TIA** | Teaching in Action |

# SURA YA KWANZA

# DIBAJI

## 1.1 Usuli

Walimu bora hubadilisha maisha. Hushajiisha. Huhamasisha. Hujitahidi kuboresha fani yao- sanaa ya ufundishaji. Walimu bora ulimwenguni hutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazomzingatia mwanafunzi [LCTs] ili kuwahusisha wanafunzi wao. Walimu hawa wanaelewa mapungufu ya kufundisha kwa mhadhara [*lecture*] ambapo mwalimu anatawala somo zima na wanafunzi wananukuu tu, na kujibu maswali machache na kuenda nyumbani kujisomea. Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazomzingatia mwanafunzi [*LCTs*] zinawahamasisha wanafunzi kuzungumza kuhusu kile wanachojifunza, kujifunza kutoka kwa wenzao na kuboresha uelewa wao na ukariri wa maudhui ya somo.

Kiongozi hiki ni kwa walimu wanaotaka kuleta mabadiliko maishani mwa wanafunzi wao, ukiwemo ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa. Ni mwongozo unaofaa wenye mbinu 70 za ufundishaji unaomzingatia mwanafunzi. Kiongozi hiki kinalenga kuwasaidia walimu kuzitumia mbinu mbalimbali ili kuboresha ufundishaji wao na ujifunzaji wa wanafunzi wao. Miongoni mwa mbinu zilizoteuliwa zimewasilishwa kwa mfumo wa video zilizotengenezwa kutoka kwa madarasa tofauti ya kitanzania ili walimu waone matumizi ya mbinu hizi katika mazingira yenye wanafunzi wengi na vifaa pungufu vya ufudishaji na ujifunzaji.

Ni pendekezo la waandishi kwamba walimu wachague mbinu moja kwa zamu na kuitumia na wanafunzi wao. Inaweza kuchukua siku au wiki kadhaa ili kuitawala mbinu hiyo na kuitumia kwa wepesi. Mbinu zenye nyota mbili (**) kwenye yaliyomo na maudhui ya kiongozi zinapendekezwa kwa walimu wanaoanza kutumia *LCTs* madarasani mwao.

## 1.2 Matumizi ya Istilahi: Ufundishaji Unaomzingatia Mwanafunzi [*LCT*]

Nchini Tanzania, maneno tofauti yanatumika kurejea '*constructivist learning'* dhana ya ujifunzaji inayochangiwa na watafiti wengi wa taaluma wanaoamini kwamba ufahamu hujengwa kupitia kuchangamana na jamii na ujifunzaji hutokea watu wanapojihusisha na utafutaji wa maarifa mapya. Misamiati inayotumika kurejea dhana hii ni pamoja na: Ufundishaji unaomzingatia mwanafunzi; ujifunzaji unaomzingatia mwanafunzi; ujifunzaji wa uulizaji wa maswali; mbinu ya ugunduzi; ufundishaji shirikishi; na ujifunzaji unaozingatia ustadi. Hiki kiongozi kitatumia 'ufundishaji unaomzingatia mwanafunzi' [*LCT*]. *LCT* ndiyo istilahi iliyotumika kwenye mafunzo na miongozo ya PZ ya awali. Pia, istilahi hiyo inatumika kwenye mafunzo ya *TIA*, mpango wa Chuo Kikuu Cha Kikatoliki cha Mwenge uliokwisha kuendesha warsha za walimu katika zaidi ya shule 100 Arusha, Kilimanjaro,Tanga na Tabora. Kwa mantiki hii istilahi ufundishaji unaomzingatia mwanafunzi imetumika kwenye kiongozi hiki ili kudumisha uthabiti wa istilahi.

## 1.3 Ufafanuzi wa Istilahi LCT

*LCT* ni mbinu ya ufudishaji ambapo wanafunzi hushiriki kikamilifu katika somo kwa kushiriki na kuzungumza na walimu pamoja na wenzao darasani. Mbinu hii hutambua kwamba wanafunzi hujifunza zaidi wanapozungumza kuhusu wanachojifunza na wengine. Kwenye madarasa ya *LCT*, wanafunzi hutumia muda mwingi kufanya mazoezi mmoja mmoja na kwa vikundi wakati wa kipindi. Mazoezi haya huhusu maarifa na stadi wanazohitaji kuzijua kwa ajili ya mitihani yao ya kitaifa, kwa ujuzi wa mtaala wa shule, na kwa maisha baada ya shule.

## 1.4 Kanuni za LCT

- Wanafunzi wanatakiwa kuhusika kikamilifu kwenye mchakato wa ujifunzaji na washiriki badala ya kuwa wasikilizaji tu darasani

- Wanafunzi wanastahili kupewa fursa tofauti ili kuwa na stadi za ngazi za juu za utambuzi katika kila darasa
- Wanafunzi wanatakiwa kuhusishwa katika uulizaji makini wa maswali na walimu wanaowapa maswali magumu au yasiyotarajiwa kuhusu mada ya kutafitiwa au maswali ambayo wanapaswa kuyajibu ili waelewe (Vavrus, 2014).

## 1.5 Faida za LCT

Kwenye mfumo wa zamani wa ufundishaji, mwalimu tu ndiye anayehusika kutoa maarifa kwa wanafunzi. Hata kama wanafunzi wanaweza kufaidi kwa kupata elimu hii, ni mara chache wanaelewa kwa nini hayo maarifa ni ya muhimu, kwa namna gani yanahusiana na ulimwengu halisi, au nini kifanyike kupitia maarifa hayo ili kuboresha jamii zao. Kwa upande mwingine, *LCT* huwahimiza wanafunzi kuuliza nini, vipi, na kwa nini, maswali ambayo lazima yajibiwe katika ulimwengu wa sasa. Kwa namna hii, kuna uwezekano mkubwa wa wanafunzi kukumbuka maarifa yaliyotolewa darasani, kuyaelewa kwa kina na kuweza kuyatumia katika mazingira halisi na mapya yanayohitaji fikra changanuzi (Vavrus,2014). *LCT* zilizotumika vizuri huhamasisha ujifunzaji, uwezo mkubwa wa kushika maarifa, uelewa wa kina, na mitazamo chanya kwa somo lifundishwalo (O’Brien, 2003). Faida nyinginezo za *LCTs* ni pamoja na:

- Kuongeza kujiamini kwa mwanafunzi
- Kuhamasisa uulizaji wa maswali na majadiliano
- Kukuza fikra pambanuzi
- Kutengeneza mazingira rafiki ya ujifunzaji , hivyo kuwafanya wanafunzi kutulia na kujifunza
- Kuwavutia wanafunzi na kuwafanya wachangie hoja ndani ya kipindi
- Kuhamasisha ujifunzaji wa msingi unaorahisisha kushika na kutumia maarifa. Hii ni tofauti na mfumo wa zamani unaokuza kukariri tu
- Wanafunzi kujifunza pekee yao, na kujifunza kujisimamia na kufanya maamuzi yao wenyewe
- Kukuza kazi za vikundi na kuwasaidia wanafunzi kuheshimu mawazo ya wenzao
- Wanafunzi kujifunza stadi muhimu za kuwasiliana na kushirikiana kupitia kwa kazi za vikundi
- Wanafunzi kujifunza kuongoza ujifunzaji wao, kuuliza maswali na kukamilisha mazoezi ya mmoja mmoja.

## 1.6 *LCT* Katika Sera za Serikali ya Tanzania

Si walimu tu, hata watunga sera wanatambua umuhimu wa *LCT* kwa uboreshaji wa ujifunzaji na matokeo ya kitaaluma. Kwa mfano, *Tanzanian Development Vision 2025* kimeandika yafuatayo:

> Taaluma inatakiwa kutazamwa kama chanzo chenye mikakati ya kubadilisha mitazamo ya watu na kujenga taifa lililoelimika vizuri, lenye maarifa yanayohitajika kwa kutatua matatizo ya maendeleo yanayolikumba taifa kwa ufanisi na ushindani. Hivyo basi, mfumo wa elimu unapaswa kuundwa upya na kubadilishwa ili ulenge kukuza ubunifu na utatuzi wa matatizo. (Uk. 19; mkazo umeongezwa)

Sera na mitaala ya *MOEVT* pia inawataka walimu watumie *LCTs* madarasani, kama vile “fikra changanuzi na bunifu,” na wawe na uwezo wa “kutumia mbinu rafiki za ufundishaji na ujifunzaji zinazowashirikisha wanafunzi katika ujifunzaji wao” (MOEC, 2004, uk. 15). Mapendekezo haya

yanaonekana mara kwa mara kwenye taarifa zinazohusu elimu ya kitanzania za '*World Bank'* na Haki Elimu, miongoni mwa mashirika mengine yanayopendekeza fikra changanuzi na mbinu za utatuzi wa matatizo zitumike kila inapowezekana katika shule za sekondari.

## 1.7 Sifa za Mwalimu Shirikishi kwa Mazingira ya Kitanzania

- Mwalimu shirikishi huwahimiza wanafunzi kufanya kazi katika vikundi vidogo vidogo ili kuongeza ushiriki na ujifunzaji wa pamoja
- Mwalimu huvaa jukumu la kusahili au kurahisisha somo ili kuhamasisha, kuongoza na kusaidia ujifunzaji wa wanafunzi
- Mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji ni shirikishi na husishi kwani mwanafunzi hujifunza kwa kufanya vitendo kadha wa kadha kama uigizaji, majadiliano, ufumbuzi wa matatizo, vitendo, majaribio, nk (MoEVT,2007).

## 1.8 Nadharia Zinazoongoza *LCT*

Zipo nadharia mbali mbali zinazounga mkono ufundishaji unaomzingatia mwanafunzi. Nadharia ya Utambuzi, Nyanja za Utambuzi za Bloom, na Nadharia ya Akili Nyingi [*Multiple Inteiligence Theory*] zimejadiliwa kwenye sura hii.

### Nadharia za Utambuzi

Dhana na mazoezi ya *LCT* vimejikita kwenye nadharia ya utambuzi. Nadharia hii inaonyesha wazi kwamba wajifunzaji hujijengea maarifa wenyewe - kila mjifunzaji mmoja mmoja (na kwa pamoja) na kujenga maana anapojifunza. Kuna matokeo mawili ya huu mtazamo. Kwanza, ni lazima mwalimu amfikirie mjifunzaji kwa mtazamo wa ujifunzaji (si somo analoenda kufundisha). Pili, hakuna maarifa yasiyo husiana na maana iliyojengwa kutokana na uzoefu wa mjifunzaji au jamii ya wajifunzaji (Hein, 1991).

Zifuatazo ni kanuni zinazoongoza nadharia ya utambuzi:

a) Ujifunzaji ni mchakato husishi ambapo mjifunzaji anatumia anachokipokea akilini ili kujenga maana

b) Watu hujifunza kujifunza wanapojifunza: ujifunzaji unahususha kujenga maana kutokana na maarifa mapya ambayo mtu hujihusisha nayo

c) Kitendo hiki muhimu cha kujenga maana ni cha kiakili- kinatokea akilini- na pia cha kijamii kupitia kwa mahusiano yetu na walimu wetu, rika zetu, jamii zetu, na watu tunaofahamiana nao. Walimu wanapaswa kutoa mazoezi yanayohusisha akili, kama vile mazoezi ya tafakuri ambayo wanafunzi wanaweza kuyafanya pekee yao, na mazoezi yanayohusisha mwili na kujenga mahusiano

d) Ujifunzaji unahusisha lugha, na hivyo basi, lugha tunayoitumia madarasani na shuleni kwa ujumla inaathiri ujifunzaji. Kadri wanafunzi wanavyoizoea lugha inayotumika shuleni, ndivyo wanavyoweza kushirikiana na kujenga maana kutokana na maarifa mapya

e) Ujifunzaji umekaa kimazingira. Tunajifunza kulingana na maarifa ya awali tulionayo (rasmi na yasiyo rasmi), tunachokiamini, upendeleo na hofu zetu (Hein, 1991).

Kanuni hizi za ujifunzaji kwa utambuzi zinadokeza kwamba ufundishaji unaweza kupelekea ujifunzaji wenye ufanisi endapo utalenga kuwafanya wanafunzi wajenge maana kutokana na kile kinachofundishwa kupitia kwa mawazo na mwingiliano na wenzao au jamii inayowazunguka.

**Nyanja za Utambuzi za Bloom**

Miaka 50 iliyopita, Benjamin Bloom na wenzake waliainisha nyanja za utambuzi ili kuelezea nyanja tatu za ujifunzaji ambazo walimu wanatakiwa wazizingatie katika ufundishaji wao. Nyanja hizo ni ufundi, mitazamo, na utambuzi.

Kwanza, ujifunzaji wa **ufundi** unalenga kuboresha uwezo wa wanafunzi wa kutumia ufundi unaoonekana, kama kutumia dira au kutumia vifaa vya maabara katika upimaji wa kisayansi.

Pili, ujifunzaji wa **mitazamo** ni pale ambapo wanafunzi wanatambua jazba zao, misimamo yao, na hisia zao. Ujifunzaji huu unaweza kuhusisha kumhamisha mwanafunzi kutoka kwenye kukaa tu darasani kwenda kwenye kupima somo, kuamua atakachokiamini na kujenga hisia kuhusu somo husika.

Tatu, ujifunzaji wa **utambuzi** ambao unasisitizwa mashuleni unahusisha upataji wa maarifa na ufahamu wa mada husika. Nyanja hii inagawa ujifunzaji katika ngazi, kuanzia ya chini hadi ya juu kabisa:

- *Maarifa*: Ngazi ya msingi katika ujifunzaji- inahusu kukariri mawazo, istilahi, tarehe, n.k.
- *Ufahamu*: Kuelewa dhana na kuzielezea
- *Matumizi*: Kutumia maarifa na stadi katika mazingira tofauti.

Hizi ngazi za ujifunzaji zinaitwa stadi za kiwango cha chini kwa sababu ni nyepesi na hazihitaji stadi za utambuzi za kiwango cha juu. Stadi za utambuzi za kiwango cha juu ni:

- *Uchambuzi:* Fikra makini zinazowataka wanafunzi wafanye mambo mengi kama kuonyesha uhusiano, kuonyesha utofauti, kubainisha, na kuhusianisha dhana au vitu viwili.

- *Uundaji: U*nahitaji kiwango cha juu cha ujifunzaji kwa sababu wanafunzi wanapaswa kuunganisha, kupangilia, kuunda, na kusahihisha kazi zao kulingana na vyanzo tofauti vya maarifa.

- *Tathmini:* Fikra changamano ambapo mwanafunzi anapaswa kutoa hoja za kuunga mkono au kupinga kitu fulani, kufanya maamuzi, kutoa tafsiri, na kubashiri matokeo.

**Nadharia ya Akili Nyingi**

Hii ni nadharia iliyoibuliwa kwenye miaka ya themanini mwazoni na Howard Gardner. Lengo la nadharia hii ni kutoa mtazamo wa uwingi wa akili, na kuimarisha dhana kwamba *kuna njia zaidi ya moja za kuwa mwerevu*. Basi, mwanafunzi asiitwe mjinga bali asaidiwe kuboresha werevu alio nao ambao haujakamilika kupitia kwa mbinu safi za ufundishaji (Vavrus, 2014).

Zifuatazo ni fafanuzi bayana za akili tisa zitokanazo na utafiti wa Gardner:

1. AKILI YA KUSOMA NA KUANDIKA - uwezo wa kuelewa na kutunga matamshi au maandishi ya lugha;
2. AKILI YA HESABU- uwezo wa kuelewa na kutumia tarakimu, fikra dhanifu na kutumia mantiki kwa utatuzi wa matatizo;
3. AKILI YA MUZIKI -uwezo wa kutunga, kuelewa na kuelezea maana zinazotokana na sauti;
4. AKILI YA KUTUMIA UWEZO WA TASWIRA-uwezo wa kuelewa, kubadilisha, na kujenga taswira au picha halisi na za kifikra;

5. AKILI YA KUTUMIA VIUNGO - uwezo wa kutumia viungo vyote vya mwili kutatua matatizo na kuunda vitu;
6. AKILI YA MAZINGIRA YA ASILI -uwezo wa kutofautisha sifa za mazingira ya asili;
7. AKILI YA UTAMBUZI WA WATU -uwezo wa kutambua, kukubali, na kuhoji hisia, imani na nia za watu wengine;
8. AKILI YA UTAMBUZI WA NAFSI -uwezo wa kujielewa kwa vitu kama kama hisia, shauku, uwezo na udhaifu, na kutumia maarifa hayo vizuri ili kuyatawala maisha ya mtu binafsi;
9. AKILI YA UWEPO WA BINADAMU -uwezo wa kuwa makini, au uwezekano wa kutatua maswali ya kina au yenye upana kuhusu uwepo wa binadamu (Christodoulou, 2009).

Huenda dhana ya akili nyingi ikaakisiwa kupitia kwa msemo huu, *Ukimpima samaki kwa uwezo wake wa kukwea mti, ataishi maisha yake yote akifikiri yeye ni mjinga.*

**1.9 Hitimisho**

Walimu wa kitanzania wanaweza kubadilisha maisha yao kwa kutumia mbinu za *LCT* madarasani mwao. Hata hivyo, baadhi ya hizi mbinu zinaweza kueleweka na kutumika kwa urahisi kuliko zingine, kwa hivyo ni vyema kuanza na mbinu moja kwanza. Jitahidi kuielewa kisha endelea na zingine. Waandishi pia wanawashauri walimu watumie ukurasa wetu wa Facebook kwenye https://www.facebook.com/TendaTeachers/ ili kupata video na habari mpya kuhusu LCTs nchini Tanzania. Mwisho kabisa, mabadiliko mashuleni mwetu yanaanza na mwalimu mmoja. Mbinu hizi zikitumika kikamilifu, zina uwezo wa kubadilisha uzoefu wa ujifunzaji na maisha ya wanafunzi wetu na hivyo, kujenga Tanzania iliyo bora kwa ajili yetu sote.

## SURA YA PILI

## KUJENGA MAZINGIRA CHANYA DARASANI

Ujenzi wa mazingira rafiki darasani ndio msingi wa ufundishaji unaomzingatia mwanafunzi. Hili limejikita kwenye dhana kwamba uhamasishaji na msaada ni vya msingi kwa mafanikio shuleni na maishani. Kama anavyoonyesha Doug Lemov kwenye kitabu chake cha *Teach Like a Champion*, "Watu huhamasishwa zaidi na mambo chanya kuliko mambo hasi. Kutafuta mafanikio na furaha kutachochea utekelezaji imara kuliko kutafuta kukwepa adhabu" (2010, uk. 204).

*LCT* imejengwa kwenye imani kuwa kujenga mazingira chanya yanayochochea ujifunzaji ni jambo la muhimu kwa kuboresha matokeo ya mwanafunzi, kuhamasisha fikra yakinifu na kusaidia vijana wadogo kufaulu shuleni. Vavrus, kwenye kitabu cha *Teaching in Action* anasema,*"*Ingawa hatuwezi kuutawala ufundishaji wa wenzetu, tunaweza kuwa mifano ya mabadiliko makubwa kwa kufanya mambo madogo madogo katika mwingiliano wetu na wanafunzi; mambo yanayowahamasisha katika kusoma kwa ajili ya furaha ya kusoma na sio kwa kukwepa adhabu" (2014). Ndani ya sura hii, tunaangalia mitazamo, imani, sifa na mazoezi ya walimu yatakayounda hali chanya darasani.

### ** Mbinu #1 Fundisha kwa Shauku

Hakuna kitu kinachoshawishi na cha kufaa kama mwalimu mwenye shauku ya kufundisha na kujifunza. Walimu bora huleta mitazamo yenye furaha, uvumbuzi, na uchanya madarasani mwao. Shauku hii inaweza kuchukua maumbo tofauti, lakini hushajiisha, kuhamasisha na kuwatia moyo wanafunzi katika ujifunzaji. Kama viumbe changamfu, tunajifunza mengi kwa kuwaangalia wanaotunzunguka. Mwalimu akiingia darasani kwa wakati (au mapema) akiwa na nguvu za kutosha , akaongea kwa sauti safi yenye mvuto (lakini si kupiga kelele) na toni yenye furaha na shauku, basi wanafunzi nao watavutiwa na somo. Kinyume chake, mwalimu akiwa na mazoea ya kuingia darasani huku amechelewa, amekereka au ana hasira, ama anatumia nguvu kidogo katika ufundishaji, wanafunzi watajifunza kwa matendo kuwa mada hiyo haina mvuto sana na haina umuhimu. Walimu lazima wajenge tabia, majibu ya hisia na mitazamo wanayotaka wanafunzi wao wajifunze. Njia moja ya kujenga shauku katika ufundishaji ni kujikumbusha kila siku kuhusu umuhimu wa kazi tunayoifanya katika kuelimisha kizazi kijacho. Kabla hujaingia darasani unaweza kujiambia, "Ninaelimisha taifa", au "Ninajivunia kuwa mwalimu." Pia, unaweza kuanza siku kwa kutafakari utendaji wako, ukijiuliza kama ulifika darasani kwa wakati; kama ulitabasamu na kutumia sauti inayoonyesha shauku; na kuongea kwa namna nzuri na yenye mvuto kwa wanafunzi wako. Kama hukufanikiwa leo, ujitahidi kuboresha kipengele husika kesho mpaka iwe kawaida kufundisha kwa shauku.

### **Mbinu # 2 Jenga kwenye Uchanya

Wanafunzi huitikia sifa kuliko adhabu, na fedheha ni adhabu ngumu kwa vijana –wanafunzi wa umri kati ya miaka 13-19 –kwa sababu hiki ndicho kipindi ambacho hisia zao za kujigundua hunajengeka. Maoni ya rika zao ni ya muhimu, na ndio maana masihara au aina zozote za dhihaka zinaweza kuwa haribifu kwa wanafunzi, hivyo kusababisha wengi kuacha shule badala ya kuona akiitwa ''mjinga'' au "mpumbavu" mbele ya wengine. Njia mojawapo ya kujenga ubora zaidi kwa wanafunzi wako ni kuanza kurekebisha majibu ya wanafunzi au tabia zao bila kutaja majina ya wanafunzi wanaokosea. Kwa mfano, unaweza kusema, "Darasa, ninataka kila mtu atulie kabla sijapitisha kifaa,'' badala ya, "Robert na Godbless, acheni kupiga kelele.'' Kama bado kuna kelele unaweza kusema, ''Wengine bado hawapo tayari kusoma.'' Ikiwa Robert na Godbless bado wanasababisha usumbufu, unaweza kuwaita mbele ya darasa uwanong'oneze kuhusu tatizo kisha uwatenganishe maeneo ya kukaa. Mbinu hii pia inaweza kutumika wanafunzi wanapofanya vibaya katika zoezi au mtihani. Vijana wanaweza kuhisi unajali ujifunzaji wao endapo utawaongelesha kwa faragha kuhusu makosa yao badala ya kuwatangaza darasani kuwa wana alama za chini zaidi au kuwachapa wale waliofeli jaribio. Tunapaswa kutambua kwamba

alama za chini katika mazoezi au tabia mbaya darasani vinaweza kutokana na sababu nyingi: ulemavu wa mwanafunzi katika masomo, shida za nyumbani kwao, au ufundishaji wetu usiofaa.

****Mbinu # 3 Onyesha Matarajio ya Juu**

Watu wengi waliofanikiwa hudalilisha utekelezaji wao kwa imani ya mwalimu mmoja katika uwezo wao wa kufanikiwa. Wanafunzi wanaotoka kwenye familia au jamii zenye matarajio ya chini kwao, kama ilivyo wakati mwingine kwa wasichana, wanafunzi wenye ulemavu au wanafunzi wa matabaka ya chini, hapo mwalimu mmoja mwenye matarajio ya juu na imani kwao anaweza kuleta mabadiliko makubwa maishani mwao. Hata hivyo, haya matarajio ya juu yanatakiwa kuandamana na matendo ya mwalimu yanayowawezesha wanafunzi kufaulu. Matarajio ya juu yanaweza kudhihirishwa kwa mabango kwenye ukuta wa darasa au vibao vyenye picha za vyuo vikuu au vyuo vizuri vya ufundi, au fungu la maneno yanayohimiza mlangoni mwa maabara ya shule kama vile, ''Utulivu tafadhali, wanasayansi wako kazini.'' Kuonyesha kazi ya mwanafunzi yenye sifa za juu ukutani au kwenye vibao vya matangazo pia ni njia ya kuonyesha wanafunzi kuwa una matarajio makubwa kwao na unajivunia kazi zao nzuri.

****Mbinu #4 Wanafunzi Wote Wanaweza Kujifunza**

Mtu yeyote aliyewahi kufanya kazi na watoto darasani anajua kwamba wanafunzi huja na uwanja mpana wa wepesi, uwezo na udadisi shuleni. Wanafunzi wengine ni wepesi wa kujifunza, na wengine huhitaji msaada mkubwa katika ujifunzaji wao. Walimu wanaotumia *LCT* huamini kwamba watoto wote wanaweza kujifunza. Imani hii ni muhimu sana. Walimu wengine ni wepesi katika kuwapuuza baadhi ya wanafunzi kwa kuwaona kama wazito, wasio na uwezo au wasiotaka kujifunza. Walimu wanaotumia *LCT* hutumia njia iliyo kinyume na hiyo. Wanajitahidi kuwahusisha hata wanafunzi wasiotaka au walio na changamoto. Endapo mwanafunzi atashindwa kujifunza kitu kwa upesi kama ulivyotarajia, unaweza kuonana naye baada ya vipindi na kufanya naye zoezi jepesi ili kubaini kama ana tatizo linaloathiri ujifunzaji wake, kama tatizo la macho. Kama shule yenu haina walimu wa mahitaji maalumu, unaweza kufanya tathmini nyepesi. Unaweza kumwambia huyo mwanafunzi aende nyuma ya darasa na afumbe macho unapoandika herufi hata tano ubaoni. Kisha mwambie afunue macho na azisome hizo herufi. Kama hawezi, yawezekana anahitaji miwani au ana tatizo la macho kama '*dyslexia*'. Unaweza kufanya zoezi linalofanana na hilo kubaini tatizo la kusikia. Unaweza kupata maelezo zaidi kwenye '*Dyslexia international'* zikiwemo kozi kahusu *dyslexia* kwa walimu (http://www.dyslexia-international.org/our-approach/) na kutoka kwa Shirika la Ulimwengu la Afya (http://www.who.int/blindness/Vision2020_report.pdf na http://www.who.int/pbd/deafness/world-hearing-day/WHD2016_Brochure_EN_2.pdf).

****Mbinu #5 Sherehekea ushindi**

Njia nyingine ya kujenga mazingira chanya ya ujifunzaji ni kusherehekea ushindi wa mwanafunzi. Hii inaweza kuchukua sura ya kutoa "heko" pale ambapo mwalimu anamtambua mwanafunzi na kushiriki ufaulu wake na darasa zima. Walimu wanapaswa kutenga muda ndani ya wiki au mwezi ili kumtambua kila mwanafunzi kwa jambo jema alilotekeleza. Ni vizuri zaidi mwalimu akimtambua mwanafunzi kwa utekelezaji wa kitu mahususi. Kwa mfano*: Yusuf aliandika insha yake bora zaidi akijumuisha sentensi tangulizi, sentensi za maelezo na sentensi hitimishi*. Sifa ja jumla kama, ''kazi nzuri, Yusuf" hazina ufanisi sana ukilinganisha na sifa mahususi kwa sababu hazimfanyi mwanafunzi au darasa kujua kilichotekelezwa. Njia za ziada za kusherehekea ushindi ni pamoja na kuonyesha kazi ya mwanafunzi, kuwaambia wanafunzi watambue ushindi wa kila mmoja afanyapo kazi katika vikundi vidogo au wawili wawili. Kwa mfano: wanafunzi wanaweza kubadilishana kazi fulani au insha na wenzao, na hatimaye kubadilishana mawazo kuhusu walichokifurahia sana kuhusu kazi hiyo.

## SURA YA TATU

## KUANDAA SOMO LINALOMZINGATIA MWANAFUNZI

Walimu wanaomzingatia mwanafunzi ni waandaaji wazuri wa masomo. Hawa huanza na hatima akilini. Huamua kile wanachotaka wanafunzi wao wakipate na wanajua watawapima vipi. Pia huandaa masomo yenye mvuto na yaliyojikita kwenye malengo mazuri yanayoweza kupimika. Hutathmini maendeleo ya wanafunzi kwenye somo. Hii ndiyo sanaa ya uandaaji - mchakato wenye ubunifu unaoweza kuwa: kujifunza kwa kutafiti, masomo ya mhadhara, na mbinu zingine mbali mbali. Sura hii inalenga kuonyesha mbinu za uandaaji wa masomo zilizoonekana kuwa na ufanisi katika masomo tofauti.

### **Mbinu #6 Masomo Yenye Hatua Kuu Tano**

Masomo yenye hatua tano yana ufanisi katika ujifunzaji. Yanahusisha hatua tano. Kwanza, walimu bora huanza somo kwa kuamsha hamu na maarifa, kuuliza maswali elekezi na kuelezea malengo ya somo. Pili, mwalimu hutoa mifano na kufundisha ujuzi na maarifa. Tatu, mwalimu huongoza mazoezi ya wanafunzi. Nne, wengi wakishayaelewa maarifa vizuri, wanafunzi hufanya mazoezi ya mmoja mmoja wakati huo akiwasaidia wale ambao bado wanahitaji msaada. Mwisho, mwalimu huhitimisha somo kwa kuwataka wanafunzi watafakari walichojifunza na kutathmini kwa haraka uelewa wao. Hatua hizi zinafanana na hatua tano za maandalio yanayotumika Tanzania. Hatua zenyewe ni Utangulizi, Ujuzi Mpya, Kuimarisha Maarifa, Tafakuri na Hitimisho.

### **Mbinu #7 Somo la Ugunduzi**

Masomo ya ugunduzi yanalenga kuwahimiza wanafunzi kushirikiana na wenzao katika kujibu maswali au kutatua matatizo kabla ya mwalimu kufundisha ujuzi au dhana. Kwenye mbinu hii, mwalimu huwapa wanafunzi maswali ili wayajadili, wayatathmini na kuyatatua ili kuwahimiza kufikiri na kutoa maamuzi yao wenyewe. Wamalizapo kazi, wanafunzi hupokezana katika kulishirikisha darasa mawazo yao. Wakati huo, mwalimu hutumia majibu ya wanafunzi kufundisha somo. Mfano, mwalimu wa hisabati anaweza kutoa swali na kuwataka wanafunzi wajibu kwenye vikundi vyao. Ndiposa wanafunzi wanatoa majibu yao na mwalimu huitumia hiyo mifano kulifundisha darasa zima jinsi ya kilijibu hilo swali.

### **Mbinu #8 Anza na Mwisho Akilini

Walimu wenye ufanisi mkubwa huanza kuandaa somo wakiwa na mwisho akilini mwao. Yaani, wanaandaa somo kwa kuanza na kile walichokusudia wanafunzi wao wajifunze na njia watakazozitumia kuwatathmini. Kwanza, wanatambua malengo ya somo. Kisha, wanaandaa njia za kutathmini ujifunzaji wa wanafunzi wao. Mwisho, wanaandaa masomo na mazoezi yatakayowaongoza wanafunzi kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa mfano, mwalimu wa Hisoria anataka wanafunzi waeleze sababu na matukio muhimu katika harakati za uhuru Tanzania. Mwalimu huyo ataanza kwa kutunga mtihani wa mada kwa kuzingatia malengo hayo. Kisha mwalimu ataandaa masomo ya kila siku. Hatimaye, mwalimu atafanya tathmini mada inapoendelea na itakapokamilika.

### **Mbinu #9 Andika Malengo ya Somo

Unapoandaa mada kwenye somo, ni muhimu kubaini na kuandika darasani malengo ya msingi yanayoweza kupimika. Wanafunzi hufaulu zaidi pale ambapo walimu huwaambia wazi wazi na mara kwa mara wanachotarajia kutoka kwao, na kuwaelezea umuhimu wa kujifunza mada husika. Kuandika malengo ya somo ubaoni na kuwasomea wanafunzi kwa lugha nzuri ya kirafiki huwasaidia wanafunzi kujenga malengo ya kufikiri na kujifunza. Malengo yenye ufanisi mkubwa yanapimika na yana maana. Kwa mfano, lengo la mada ya njeo za vitenzi katika kidato cha kwanza somo la Kiingereza linaweza kuwa “kutumia wakati uliopo vizuri angalau kwa 90% katika insha zenu” au “kubaini mifano katika wakati uliopita iliyo sahihi na isiyo sahihi kwenye mazoezi na mitihani kwa asilimia 75%.

## SURA YA NNE

## LCTS MWANZONI MWA SOMO

### 4.1 Ndoano

Ndoano ni shughuli za mwanzoni mwa kipindi. Ndoano huvuta usikivu wa mwanafunzi. Inamdokezea mwanafunzi mada anayoenda kujifunza kwenye kipindi, na kuihusianisha na kile anachokijua.

****Mbinu #10 Jedwali la KWL**

Kirefu cha KWL ni Jua [*K*now], Taka kujua [*Want to know*], na Ulichojifunza [*Learned*]. Hii ni mbinu nzuri inayomsaidia mwanafunzi kukitambua kile anachokijua. Kutoka hapo, walimu wanaweza kuendelea kutokana na kile walichogundua wanafunzi wanakijua ili kuongeza mvuto na kuepuka kurudia kile wanachokijua, na badala yake kutumia muda wa kipindi kwa kile ambacho wanafunzi wanahitaji kukijua.

| K | W | L |
|---|---|---|
| | | |

****Mbinu #11 Tatizo katika Mazingira ya Kawaida**

Hii ni kwa ajili ya kuhusisha somo na uzoefu uliopo. Mwalimu anaweza kuwataka wanafunzi watatue tatizo linalohusu malengo ya somo kabla ya kuwasilisha mada ya siku hiyo. Mfano, kabla ya kufundisha *parallelogram* mwalimu wa Hisabati anaweza kuwauliza wanafunzi swali lifuatalo: "Anna, Muhammad, Asha, na Ibrahim wanaishi katika pembe nne za ghorofa. Anna anaishi mita hamsini kutoka kwa Asha. Kama pande zote mbili ni sambamba, Muhammad na Ibrahim wanaishi umbali gani mmoja kutoka kwa mwingine?"

****Mbinu #12 Simulia Kisa**

Simulizi fupi yenye mvuto inayohusiana moja kwa moja na malengo ya mada ni njia nzuri ya kuwafikirisha wanafunzi kuhusu mada husika. Inakuwa bora zaidi endapo simulizi hiyo ni sehemu ya maisha ya mwalimu na inaonyesha kwa ucheshi kwamba mwalimu, kama wanafunzi, hufanya makosa lakini amejifunza kutoka nayo. Kwa mfano, mwalimu wa Giografia anaweza kutoa kisa kuhusu alivyopotea kwa sababu hakuwa na dira, ndipo aanze kufundisha namna ya kutumia kifaa hiki muhimu kwa kutafuta mwelekeo.

**Mbinu #13 Andika Upesi**

Hii ni mbinu ya kuandika upesi inayoweza kukusaidia kujua anachokijua mwanafunzi kuhusu mada ya siku. Kwa mfano, somo la kwanza kwenye mada ya Dunia linaweza kuanza na swali kama:"Je, dunia imekuwa na muonekano huu tangu zamani? Kama sivyo, imebadilika vipi? Ilibadilishwa na nini?"

**Mbinu #14 Kanda ya Picha au Sauti**

Mwalimu anaweza kutumia kanda inayohusiana na malengo ya somo ili kuwavutia wanafunzi na kuibua majadiliano mafupi kabla ya somo. Kwa mfano, mwalimu wa Kemia anaweza kutumia video inayoonyesha matokeo ya kuchanganya sodiamu na maji.

**Mbinu #15 Barometa ya Jamii**

Mwalimu huandika ubaoni wazo ambalo wanafunzi wanaweza kukubaliana nalo, kulikataa au kuwa kati kati. Wanafunzi hutengeneza barometa darasani kwa kutumia miili yao kwa kufanya upande mmoja wa darasa 'kukubali' na mwingine 'kukataa' na upande mwingine wa 'kati kati' baada ya kusoma wazo darasani. Wazo atakaloliwasilisha mwalimu linapaswa kuwa wazo linalokubali majibu ya kujieleza. Mfano, mwalimu wa Uraia anayefundisha kuhusu Demokrasia anaweza kuandika wazo lifuatalo,"Uchaguzi mkuu Tanzania unafuata taratibu za kidemokrasia". Baada ya hapo, wanafunzi watasogea kwenye maeneo waliyoelekezwa yanayoonyesha kukubali au kukataa au kutokuwa na upande kulingana na maoni yao. Wanajadili na wenzao kwenye kikundi na mwishowe kutoa mjibu yao kwa wale wanadarasa wenye mawazo tofauti.

**4.2Vivunja Barafu**

Hizi ni shughuli zinazovunja 'barafu' au kuvunja ukimya kati ya watu wasiofahamiana waliokusanyika katika chumba. Shughuli hizi huwasaidia wanafunzi; kujua majina ya wenzao darasani na kitu kuhusu historia zao, njozi zao, ndoto zao, au maoni yao kuhusu mada itakayojadiliwa darasani au mafunzoni. Filosofia ya utumiaji wa vivunja barafu ni kwamba watu hujifunza vizuri zaidi kwenye mazingira ambayo yanawaweka huru na watu wanao wazunguka (Vavrus, 2011).

**Mbinu #16 Mnyororo wa Majina**

Mwalimu huwaweka wanafunzi kwenye vikundi vya watu 8-10. Mtu wa kwanza huanza kwa kusema jina lake na kitu akipendacho. Mfano, "Jina langu ni Anna. Ninapenda Fizikia." Mtu wa pili kwenye kikundi anarudia alichokisema Anna na kuongeza sentensi nyingine. Mfano, "Jina lake ni Anna. Anapenda Fizikia. Jina langu ni Janeth. Ninapenda Kemia." Mtu wa tatu anarudia waliyoyasema wawili wa kwanza na kuongeza sentensi ya tatu. "Jina lake ni Anna. Anapenda Fizikia. Jina lake ni Janeth. Anapenda Kemia. Ninaitwa Benjamin. Ninapenda Uraia". Mchezo unaendelea na wanafunzi wengine kwenye kikundi.

**Mbinu #17 Nisahili**

Mwalimu huwagawa wanafunzi wawili wawili, au kila mwanafunzi humchagua yule asiyemfahamu vizuri (yaani, mtu asimsahili rafiki yake wa karibu). Wanafunzi wawili wawili huhojiana kwa dakika tatu hadi tano kwa siku ya kwanza darasani. Mwalimu anaweza kuandaa maswali halisi kabla ya kipindi , kwa mfano "Unaitwa nani?" au "Ulizaliwa katika wilaya ipi?" Vile vile, mwalimu anaweza kutoa mwongozo wa mahojiano hayo, kama "ujue mambo matatu kuhusu familia ya mwenzako [au kuhusu mchezo aupendao au kitu anachopenda kukifanya]." Baada ya mahojiano, mwalimu huwakusanya wanafunzi na kuchagua baadhi ya wanafunzi wa vikundi tofauti tofauti ili wawatambulishe wenzao kwa darasa lote.

**Mbinu #18 Mchezo wa Kweli Nne (Moja si Kweli)**

Kila mtu huandika kweli tatu hadi nne kumhusu, na moja isiyo ya kweli. Baadaye kila mtu huchukua nafasi kusoma orodha yake kwa sauti na wenzake darasani wanaandika kile wanachohisi ni cha uongo. Wote wamalizapo kusoma orodha zao, mtu wa kwanza hurudia kusoma orodha yake na kuonyesha kile ambacho si cha kweli. Mchezo unaendelea na washiriki wengine wakionyesha vitu vya uongo kwenye orodha zao na wanadarasa wakikagua usahihi kukisia kwao.

**Mbinu #19 Kuonyesha Vipaji**

Kila mwanafunzi darasani huchagua kipaji au talanta yake ambayo anaweza kuionyesha darasani. Wanajitambulisha, wanaelezea vipaji vyao, na kuvionyesha darasani. Kwa madarasa makubwa, mwalimu anaweza kuchagua wanafunzi watatu hadi wane kila siku au mara moja kwa juma ili wote waonyeshe talanta zao ndani ya muhula.

Huu ni mchezo mzuri wa kusalimiana kwa wanafunzi wanaokutana kwa mara ya kwanza (mf. wanafunzi wa kidato cha kwanza au cha tano). Wanafunzi hutengeneza duara mbili, moja ikiwa ndani ya nyingine. Wanafunzi kwenye duara ya ndani huwageukia wale wa duara ya nje. Mwalimu huwaelekeza wanafunzi kupiga hatua kinyume na wenzao ili kila mmoja akutane na mtu mgeni kadri duara inavyoendelea kusogea taratibu na wanaendelea kujitambulisha.

## SURA YA TANO

## MBINU ZA UULIZAJI MASWALI

Walimu bora hutumia njia mbalimbali za uulizaji maswali kuwahusisha wanafunzi wao na kuboresha ujifunzaji wa mwanafunzi. Changamoto ni kutafuta njia za kuwahamasisha wanafunzi wote kujibu maswali katika vichwa vyao au kwa faida ya wengine darasani. Njia ya kawaida na iliyozoeleka kutumika ni kuuliza swali na kuchagua mwanafunzi kati ya walionyosha mikono, lakini lazima iunganishwe na mbinu zingine ili kuongeza ujifunzaji kwa wanafunzi wote, hata kwa ambao hawakuchaguliwa au hawakunyosha mikono yao. Sehemu hii itahusisha mbinu za uulizaji maswali kumi na mbili (12) ambazo mwalimu makini hutumia kuwahusisha wanafunzi. Tunakuhimiza utumie mbinu angalau mbili za uulizaji maswali katika kila kipindi na ujaribu mbinu mpya mara moja katika kila mada kwenye mtaala.

****Mbinu #21 Hakuna Mikono**

Mbinu hii inamaanisha kuwachagua wanafunzi wasionyosha mikono. Walimu makini hutumia mbinu hii kwa kuwatangazia au bila kuwatangazia wanafunzi. Hili hufanyika ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anajua kwamba anaweza kuchaguliwa muda wowote. Kwa namna hii, hawawezi kuacha kushiriki kwa kutonyosha mikono. Ikitumika mara kwa mara, mbinu hii ina ufanisi mkubwa kwa kuwafanya wanafunzi wasikilize na kujihusisha. Hata hivyo, ikiwa mwanafunzi hafahamu kabisa jibu, mwalimu anatakiwa amuulize mwanafunzi mwingine ili asimfedheheshe yule aliyeshindwa kujibu.

****Mbinu #22 Muito na Muitikio**

Mwito na kujibu ni njia ambayo walimu wameitumia kwa vizazi vingi. Mwalimu huuliza swali na wanafunzi wote(darasa) hujibu kwa pamoja. Wakati mwingine mwalimu hutumia ishara kwa kuwauliza wanafunzi kwa kusema “Wote!” ili kuwaongoza wote wajibu kwa pamoja. Njia hii huhamasisha na kutoa nafasi kwa kila mwanafunzi kujibu swali lililoulizwa.

****Mbinu #23 Uliza Tena**

Hii inatumika pale ambapo mwanafunzi anatoa jibu lisilo sahihi au kusema “Sifahamu.” Mwalimu hujibu kwa kusema , “Nitarudi tena unipe jibu, kwa hiyo sikiliza majibu ya wenzako.” Mwanafunzi mwingine apatapo jibu sahihi, mwalimu humrudia yule wa kwanza na kumuuliza tena lile swali ilia toe jibu. Faida za mbinu hii ni kwamba inahamasisha usikivu na kumpa mwanafunzi ujumbe kwanza atajifunza kitu.

****Mbinu #24 Rahisisha Swali**

Njia hii hutumika pale mwanafunzi anaposhindwa kujibu swali. Mwalimu humhamasisha mwanafunzi kujibu swali kwa kutoa ufafanuzi wa swali na kulifanya liwe rahisi na kisha huandaa madokezo ya kumsaidia mwanafunzi kutengeneza majibu. Uhamasishaji huo humfanya mwanafunzi afanikiwe kujibu swali kwa ufasaha, humjengea kujiamini na kuboresha uelewaji wake. Zaidi ya hapo, wanafunzi wengine ambao hawakujua jibu wanaweza kujifunza kwa njia hii. Kwa mfano: mwalimu anauliza je neno *nyumba* ni nomino? Mwanafunzi anajibu *sifahamu.* Hapo mwalimu anaweza kumuuliza nini maana ya nomino. Mwanafunzi aseme ni mtu, mahali au kitu. Kisha mwalimu aulize kama nyumba ni mtu, mahali au kitu. Mwanafunzi ajibu ni kitu. Ndipo mwalimu aulize swali lake la awali. Kwa hiyo je nyumba ni nomino? Kufikia hapo, kuna uwezekano mkubwa wa mwanafunzi kutoa jibu sahihi.

****Mbinu #25 Nielezee Zaidi**

Mbinu hii ya uulizaji maswali huwahamasisha wanafunzi kupanua mawazo yao na kufikiria kwa kina kuhusu swali au mada. Inatumika pale ambapo mwanafunzi anajibu swali kwa ufasaha na mwalimu anamuuliza aelezee zaidi kuhusu mada, au anamuuliza swali la ziada la kumsaidia kufikiri zaidi kuhusu mada au kutumia Nyanja za juu za utambuzi – kama kulinganisha na kutofautisha, kutathmini,

kuunganisha mawazo, na ufupisho. Kwa mfano, kwenye kipindi cha Biolojia kuhusu visababishi vya uchafuzi wa maji, mwanafunzi anaweza kutaja mbolea zinazotu,ika na wakulima na baadaye kuoshwa kwenda mtoni mvua inaponyesha. Mwalimu anaweza kumtaka mwanafunzi atathmini njia mbadala za matumizi ya mbolea au kuunganisha mawazo kuhusu uchafuzi wa maji kwenye kipindi hiki na matumizi ya mbolea za asili zilizojadiliwa katika kipindi cha awali.

****Mbinu #26 Kubali au Kataa**

Mbinu huanza na kitendo cha mwalimu kuuliza swali. Mwanafunzi hujibu. Ndipo mwalimu hulitaka darasa likubali au kukataa. Mwalimu anaweza kusema, “Kama unakubali, liza vidole mara mbili,” au onyesha dole, au inua mkono juu.” Kubali au Kataa hutumika kuwahamasisha wanafunzi wote kutathmini jibu na kwa walimu kupima uelewa. Ni vyema zaidi endapo mwalimu atawachagua wanafunzi watetee hoja. Hii husaidia kuhakikisha kwamba wanafunzi hawakubali kwa kufuata mkumbo.

****Mbinu #27 Swali la Siku**

Hili ni swali ambalo mwalimu huliandika kila siku ubaoni kwa malengo ya kujifunza. Ni swali ambalo walimu huwataka wanafunzi kulijibu kwa usahihi kila mwisho wa kipindi au somo. Mwalimu huwafikirisha swali hilo mwanzoni mwa somo na humaliza somo kwa kuwataka wanafunzi walijibu. Ifuatayo ni mifano ya masomo mbali mbali: Biolojia: Ujangili una athari gani kwa mazingira ya Serengeti? Fizikia: Elezea tofauti kati ya uzito na ujazo Uraia: Ni nini maana ya serikali ya mfumo wa bunge?

****Mbinu #28 Maswali ya Wote**

Maana yake ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wa kike na wa kiume, wenye uelewa wa haraka au uelewa wa pole pole, na wanafunzi wa kila kabila, dini na wanaotoka katika mazingira tofauti tofauti wanajibu maswali. Ni lazima mwalimu ahakikishe anawachagua wanafunzi wote kujibu maswali kwa muda. Hapa, wewe kama mwalimu unatakiwa kujitathmini mwishoni mwa kipindi kuhusu wanafunzi uliowachagua na wale ambao hukuwachagua kujibu maswali. Unagundua viashiria vinavyoonyesha kwamba yawezekana unawapendelea baadhi ya wanafunzi kuliko wengine? Kama ni ndio, siku nyingine jitahidi kuwahusisha wanafunzi wote kwenye ujibuji wa maswali.

****Mbinu #29 Uliza Maswali ya Nyanja za Juu za Utambuzi**

Walimu wanaweza kuwahusisha wanafunzi wenye ufikiri tofauti tofauti kwa kuwauliza maswali sahihi. Nyanja za Utambuzi za Bloom zinatambua ngazi sita za kufikiri. Zifuatazo ni fafanuzi za za ngazi hizo na maneno yanayotumika katika kutahini wanafunzi. **Kukumbuka** (ngazi ya kwanza): Wanafunzi hutafuta au kukumbuka taarifa. Walimu wanaweza kutumia maneno haya wanapowauliza wanafunzi maswali: *taja, orodhesha, onyesha, tambua, toa sifa -a, kariri, toa maana ya, au toa mawazo*. **Ufahamu** (ngazi ya pili): Wanafunzi huelewa taarifa na kuzielezea. Walimu wanatakiwa watumie maneno yafuatayo katika kuuliza maswali yao: *elezea, fupisha, jadili au fafanua*. **Matumizi** (ngazi ya tatu): Wanafunzi hutumia taarifa katika jambo au hali mpya. Walimu wanatakiwa kutumia maneno yafuatayo katika kuuliza maswali yao: *tumia, tatua tatizo, chora ramani au mchoro, na tumia taarifa.* **Uchambuzi** (ngazi ya nne): Wanafunzi huchambua taarifa na kuchunguza uhusiano wa dhana. Walimu wanatakiwa watumie maneno yafuatayo katika kuuliza maswali yao: *ainisha, chunguza, linganisha na kutofautisha, au unganisha*. **Tathmini** (ngazi ya tano): Wanafunzi huchambua taarifa na kufanya maamuzi. Mwalimu anatakiwa kutumia maneno yafuatayo kuuliza maswali: *tathmini, pima, pima kwa hoja, tetea, na kosoa*. **Uundaji** (ngazi ya sita): Wanafunzi hutumia taarifa kuunda kitu kipya. Walimu wanatakiwa watumie maneno yafuatayo katika kuuliza maswali: *tengeneza, jenga, tunga, panga, zalisha, buni, au vumbua*.

****Mbinu #30 Maswali ya Upesi**

Hii ni mbinu ya kuuliza maswali haraka haraka na wanafunzi hawanyoshi mikono yao. Mwanafunzi akijibu ipasavyo, mwalimu husonga mbele kuuliza swali jingine. Mwanafunzi akikosa, mwanafunzi huenda kwa mwanafunzi mwingine ili kupata jibu sahihi. Hii ni chemsha bongo nzuri kwa kipindi. Kwa kawaida, ni zoezi fupi linalochukua dakika chache tu. Zoezi hili hujenga mazingira kama ya mchezo darasani na kuwahamasisha wanafunzi kuwa makini. Wanafunzi wanaweza kusimama ili kuleta uchangamfu wakati wa zoezi.

**Mbinu #31 Subiri Muda**

Unapouliza maswali, mara nyingi ni wazo zuri kuwapa wanafunzi muda wa kutosha - kama sekunde 5 hadi 7 za kufikiria kuhusu jibu kabla ya kuwapa msaada. Mara nyingi walimu hukimbilia haraka kwa mwanafunzi mwingine ili kuondoa hali ya ukimya hivyo, kutowapa wanafunzi muda wa kutosha kufikiria jibu.

**Mbinu #32 Ipate Sawa sawa**

Mbinu hii humsukuma mwanafuzi ajibu swali kwa usahihi, pale jibu lake linapokuwa karibu na jibu sahihi. Mwanafunzi akijibu karibia na usahihi wa jibu, mwalimu anasema, "Umebakiza kidogo upate jibu sahihi." Kisha mwalimu humuuliza tena yule mwanafunzi au mwanafunzi mwingine darasani kutoa majibu sahihi zaidi.

**Mbinu #33 Maswali Rejeshi**

Walimu makini huanza somo kwa kuuliza maswali ya somo lililopita ili kuwasaidia wanafunzi kuunganisha mawazo yao na somo lililopita. Mara nyingine maswali ya somo lililopita huandikwa ubaoni ili wanafunzi wayajibu wanapoingia darasani na kukutana nayo. Pia maswali rejeshi hutumika kuwaandaa wanafunzi kwa jaribio au mtihani. Maswali haya yanaweza kuulizwa kwa namna zifuatazo: "Jana tulijifunza kuhusu njia za uchafuzi wa maji. Ni nani anayeweza kutukumbusha mojawapo ya njia hizi?" [mchague mwanafunzi mmoja] "Mwingine anayekumbuka njia nyingine?" [mchague mwanafunzi mwingine na kuendelea hadi hapo mawazo makuu yatakapokuwa yamerejelewa]

## SURA YA SITA

## LCTS KWA MAENDELEO YA MAARIFA MAPYA NA UIMARISHAJI

Sura hii inaelezea LCTs fasaha kwa ujenzi wa maarifa mapya na hatua za uimarishaji wa somo. Baadhi ya mbinu zilizojadiliwa katika sura ya tisa na ya kumi zinaweza kutumika katika hatua hizi mbili za somo.

****Mbinu #34 Utafiti Maalum**

Wanafunzi hupewa simulizi ya kisa cha maisha halisi ambacho hutengeneza tatizo ua jambo lisilo tatulika ambalo wanafunzi wanaweza kuchanganua, kuchunguza na kutatua. Utafiti maalum ni tofauti na kazi nyingine za vikundi kwa sababu unahusisha tatizo lenye changamoto linalosadifu maisha halisi. Kupitia utafiti maalum, mwalimu ana nafasi ya kuwaonyesha wanafunzi ni kwa namna gani wanaweza kutumia taarifa wanazojifunza darasani. Hii husababisha yaliyojadiliwa kueleweka zaidi kwani wanafunzi huyahusisha na maisha halisi. Utafiti maalum katika somo la Uraia kidato cha Pili kwenye mada ya Jinsia waweza kuhusisha uchambuzi wa kisa cha unyanyasaji wa kijinsia kilichoandikwa kwenye gazeti nchini Tanzania.

****Mbinu #35 Kila mtu Anaandika**

Mbinu hii huhamasisha wanafunzi kuandika majibu yao kwanza kabla ya kuongea na kuwashirikisha wenzao. Mwalimu huuliza swali na kuwaelekeza wanafunzi kuandika jibu fupi. Kisha mwalimu huwaambia wanafunzi kushirikishana walichokiandika au huwaambia wanafunzi kubadilishana majibu yao na kushirikiana na mwanafunzi mwenzake au kikundi kidogo. Mbinu hii huwasaidia wanafunzi kujijengea uwezo wa kuandika na kufafanua fikra zao. Pia mwalimu anaweza kuwahamasisha wanafunzi kutumia misamiati fulani au vipengele muhimu katika uandikaji wao.

****Mbinu #36 Sentensi Anzilishi**

Sentensi anzilishi ni sentensi ambayo mwalimu huandika na kumuelekeza mwanafunzi kuimalizia. Inatumika kusaidia wanafunzi kuimarisha uandikaji wao na kufikiri kwao juu ya mada tajwa. Mbinu hii husaidia kwa wale waandishi wanaohangaika namna ya kuanza kuandika sentensi. Ikifanywa kwa ubunifu, sentensi anzilishi inaweza pia kumuelekeza mwanafunzi kufikiri na kumsaidia kuelewa vizuri lengo la ujifunzaji. Kwa mfano, mwalimu wa Kiswahili anayewasilisha mada ya mithali anaweza kuandika sentensi anzilishi ifuatayo na kutaka wanafunzi waimalizie: "Mtu ni watu maanake…" Mwalimu anaweza kuchagua baadhi ya wanafunzi watoe majibu yao darasani.

****Mbinu #37 Kuta za Maneno**

Kila somo lina istilahi na maneno makuu ambayo mwanafunzi anatakiwa ayajue ili kuelewa malengo ya somo. Maneno haya na dhana yanapaswa kufundishwa na kurudiwa kila siku na kuandikwa kwenye sehemu ya "ukuta wa maneno" ubaoni. Misamiati yaweza kurudiwa au kufundishwa mwanzoni mwa kipindi na kuachwa ubaoni na ajili ya marudio ya baadaye. Wanafunzi wanaweza kuelekezwa kutumia ubao wanapojibu maswali au kujadiliana na wenzao. Walimu wazingatie kuweka maswali ya misamiati katika mitihani na majaribio.

****Mbinu #38 Vikomo vya Muda**

Walimu wanapotoa kikomo cha muda wa kumaliza kazi, inawaonyesha wanafunzi kuwa muda wa darasani ni wa thamani na unatakiwa utumiwe vizuri kadiri iwezekanavyo. Inaweza kubadilisha kasi ndani ya darasa kutoka taratibu kwenda haraka kwa kusema, "Haya, mna dakika tatu za kufanya kazi hii. Tayari, tulia, anza!" Vikomo vya muda pia ni njia nzuri itakayowasaidia wanafunzi kufanya kazi ambazo hutumia muda mwingi wa darasani kama vile kugawa vitabu, karatasi, kwa kumwagiza mwanafunzi aliye mbele na mwishoni mwa kila msitari kugawa vitabu au karatasi haraka na kwa uangalifu kadiri

iwezekanavyo. Wanafunzi wanaobaki kwenye msitari lazima wapitishe vitabu na makaratasi haraka iwezekanavyo, na kwa kufanya hivyo wanaokoa muda na si mwalimu kupita akigawa vifaa hivyo. Mwalimu anaweza kufanya kama shindano mwanzoni: "Ni mstari upi utapitisha vitabu haraka na kwa uangalifu zaidi, yaani bila kuangusha wala kuchana? Haya tuanze, 10-9-8-7…" Kisha mwalimu huwapongeza wanafunzi wa msitari uliofanya haraka na ndani ya wiki chache, wanafunzi watakuwa wameshajifunza namna ya kupitisha vifaa vizuri bila ya mwalimu kuhusika.

****Mbinu #39 Mwanzo Mzuri**

Kama ilivyosemwa awali, mwalimu aliyekusudia kutumia kila dakika ya kipindi kusababisha ujifunzaji huweka zoezi ubaoni- swali la kujibu, msamiati wa kutumia katika sentensi, swali la hisabati- ili wanafunzi washughulike mwalimu anapoandika kitu kingine ubaoni, au kupangilia vyanzo vya somo la siku. Mwalimu anaweza kutenga upande mmoja wa ubao kwa ajili ya mazoezi yanayosababisha *mwanzo mzuri*, mazoezi yanayowasaidia wanafunzi kufikiria kuhusu somo mara tu mwalimu aingiapo darasani na mara nyingine kabla ya wanafunzi wengine kuingia. Walimu wanaweza kuwasifia wale wanafunzi wanaokamilisha hili zoezi kila siku na kuwatumia kwa kusahihisha zoezi la kipindi kilichopita au kuangazia somo la siku hiyo.

**Mbinu #40 Mhadhara Shirikishi**

Hii ni moja ya mbinu bora za mbadala kwa kufundisha mada mpya na ngumu. Njia ya mhadhara shirikishi inaweza kufanywa kwa njia tofauti tofauti kama vile kuwapa wanafunzi maswali ya kujibu mwishoni mwa kipindi; kuacha nafasi za wanafunzi kujaza wakati mwalimu anafundisha mada; mwalimu kutulia kwa dakika 1 mpaka 5 ili wanafunzi wajibu swali, kutoa maoni, kujadili mada wawili wawili, na kadhalika. Chaguo zote tatu zinakusudia kuelekeza akili za wanafunzi kwenye mada iliyowasilishwa. Mwisho wa mhadhara, mwalimu hufafanua vipengele vilivyowakanganya wanafunzi na kusahihisha taarifa zisizo sahihi. Ikiwezekana, wanafunzi wahusishwe kutoa majibu sahihi ya maswali yaliyotolewa darasani. Ikiwezekana, waombe wanafunzi kufafanua majibu yao.

**Mbinu #41 Kuonyesha Kazi za Wanafunzi kwa Ujifunzaji**

Hii huhamasisha usomaji wa mtu mmoja mmoja kwa kutumia nyanja za juu za utambuzi kama tathmini na kuunganisha, na kukomboa muda wa vipindi unaohitajika kufundisha na kujifunza dhana na misingi migumu lakini ya msingi. Wanafunzi huelekezwa kusoma mifano mipya ya dhana iliyofundishwa darasani kwenye vitabu husika vya kiada mathalan, mifano ya nchi zenye serikali za kidemokrasia nchini pale mwalimu anapogundua kuwa amelenga dhana ya demokrasia yenyewe darasani. Mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi waandike kuhusu mifano kadhaa ili wawashirikishe wenzao kwa kuandika mabango ya mada husika na kuyabandika kwenye ukuta darasani ili wenzao wasome. Vile vile, mwalimu anaweza kuwataka wanafunzi wasome mabango ya wenzao kwa kuwapa zoezi fupi. Mkakati huu unawasaidia wanafunzi wazoee kujisomea na kujifunza kwa wenzao.

**Mbinu #42 Kutembelea Vituo vya Maonyesho**

Hii ni mbinu bora ya kupitia mada nyingi au kuonyesha matumizi mengi kutoka kwenye wazo au kanuni moja kwa njia ya kufurahisha sana kwa wanafunzi. Mwalimu huandaa kikundi cha wanafunzi (walimu-mbia) kulingana na idadi ya vipengile katika mada ya kujadiliwa. Kila mwalimu-mbia hupewa muda wa kutosha kusoma na kuandaa michoro, picha na vielelezo vinavyohitajika katika kuelezea kipengele chake vizuri. Wakati wa somo, kila mwalimu-mbia husimama sehemu tofauti na vifaa vyake vya kujifunzia alivyoviandaa, tayari kwa kutoa maelezo juu ya kipengele alichopewa kwa wanafunzi wenzake. Njia hii ina ufanisi zaidi pale mwalimu anapowapa wanafunzi maswali ya kujibu wakiwa wanatembea na sio kusimama mahali pamoja.

Mbinu hii ina changamoto mbili. Moja, inahitaji nafasi ya kutosha. Madarasa madogo yenye madawati yaliojaa hayawezi kufaa kwa mbinu hii. Changamoto ya pili ni kuwasimamia wanafunzi wakati wa maonyesho. Wanafunzi wote hawawezi kuwa sehemu moja kwa wakati mmoja. Inabidi wagawanywe katika vituo tofauti tofauti na mwalimu atenge muda wa wanafunzi kukaa katika kituo kimoja na kuenda kwenye kituo kingine. Ni muhimu kutumia kipenga au kengele kuonyesha kwamba ni muda wa kuenda kwenye kituo kingine.

**Mbinu #43 Mazoezi ya Mmoja Mmoja**

Huu ni muda wa wanafunzi kufanya mazoezi wenyewe. Ni muda mzuri pia kwa walimu kuwasaidia wanafunzi wanaohangaika kwenye vikundi au mmoja mmoja. Mwalimu shirikishi hatumii muda huu kwa ajili ya kuwapa wanafunzi alama au kukaa tu kwenye dawati bali huutumia kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji msaada.

**Mbinu #44 Imla**

Imla ni mbinu ya ujifunzaji ambayo imetumika kwa vizazi na vizazi. Mwalimu husoma neno, sentensi, au habari na wanafunzi huandika walichokisikia. Hii huwapa wanafunzi fursa ya kujifunza istilahi mpya na kufanya mazoezi ya usikilizaji, tahajia na uandikaji. Wanapomaliza, wanafunzi hukagua kazi zao kwa kuzilinganisha na habari ya kwanza.

**Mbinu #45 Egesho la Maswali**

Katika darasa linalomzingatia mwanafunzi, wanafunzi huhamasika kuuliza maswali kwa mwalimu na kwa wanafunzi wenzao ili kuhakikisha kuwa wanaelewa somo. Hata hivyo, mwanafunzi anaweza kuuliza swali lisiloendana na mada ya siku hiyo au akagusia mada inayotakiwa kujadiliwa kesho yake. Kwa wakati mwingine, italeta maana ikiwa swali hilo litajibiwa kwa usahihi, na ikiwa wanafunzi wengine wataonyesha hali ya kuuliza swali hilo. Wakati mwingine, itakuwa bora zaidi ikiwa swali hilo litajibiwa mwishoni au siku inayofuata ya mada husika. Katika mazingira hayo yote mwalimu anaweza kuandika swali kwenye kona ya ubao na katika andalio lake la somo kwenye ”tathmini/ maoni” ili kumwezesha kukumbuka swali hilo - katika kijisehemu kiitwacho *Egesho la Maswali* ambapo maswali huhifadhiwa mpaka yatakaporudishwa darasani kwa kujadiliwa. Unaponakili maswali ya wanafunzi kwa ajili ya mjadala wa baadaye, unawathibitishia kuwa unayapa maswali yao umuhimu mkubwa na kwamba utayajibu ingawa si kwa muda huo.

## SURA YA SABA

## KAZI ZA WAWILI NA VIKUNDI

Walimu wanaotumia ufundishaji wa LCT mara kwa mara hutengeneza fursa kwa wanafunzi wao kufanya kazi wawili wawili au kwenye vikundi. Utafiti unaonyesha kwamba wanafunzi wanaweza kujifunza zaidi na kutunza kumbukumbu ikiwa watapata fursa za kujadili kile wanachojifunza. Hii huwasaidia katika ufaulu wao na, wakitumia mbinu nzuri za uulizaji maswali, uelewa wao utakuwa mpana na wa kina.

### 7.1 Kazi za Wawili Wawili

Kazi za wawili wawili zinaweza kufanyika muda wowote wa kipindi. Zinaweza kufanyika katika somo lolote lile. Wanafunzi wanaweza kujadili, kutoa maoni yao kuhusu kazi iliyoandikwa, kusoma pamoja na kusaidianakukamilisha zoezi muda wa mazoezi ya kuelekezwa wakati wa kipindi.

Zoezi hili linakuwa na ufanisi mkubwa pale ambapo walimu huwaonyesha wanafunzi jinsi ya kufanya kazi na wenzao na kutoa utaratibu wa kutafuta wenza wa kufanya nao kazi. Hivi, kazi ya wawili wawili inakuwa nyepesi na yenye ufanisi. Matarajio kama sauti za chini, kupokezana, na kuongea na wenzao tu na sio wengine, na kutii viashiria vya kimya ni mifanoya tabia zinazotarajiwa kwenye hili zoezi.

#### **Mbinu #46 Geuka na Zungumza

Hata kama baadhi ya wanafunzi hujifunza vizuri kwa kusikiliza, kwa wengine inakuwa vyepesi kwao kujifunza katika mazingira shirikishi. Kwa hivyo, itawasaidia wanafunzi wengi mwalimu akiuliza swali na kutulia ili wanafunzi walitafakari kidogo baada ya kila dakika kumi za kipindi. Baadaye mwalimu huwaongoza wanafunzi kugeukiana na kuzungumza na wale waliokaa jirani nao. Wanafunzi hupokezana kushirikishana mawazo yao. Hatimaye, mwalimu huwanyamazisha na kuomba baadhi yao watoe mawazo yao darasani. Mbinu hii humpa kila mwanafunzi fursa ya kufikiri na kujibu swali. Vile vile, huhamasisha majadiliano na kuwasaidia wanafunzi kusaidiana kujibu maswali au kuuliza maswali ambayo hawawezi kuyauliza mbele ya darasa.

#### **Mbinu #47 Fikiri-Ungana-Shirikishana

Mbinu hii inafanana na ile ya Geuka na Zungumza. Mwalimu huwasilisha mada ya mjadala kwa njia ya swali, na wanafunzi hujadili wawili wawili yanayoweza kuwa majibu. Wanafunzi hupewa muda (dakika moja hadi mbili) mmoja mmoja wafikirie kuhusu mada kisha waungane wawili wawili ili kujadili swali hilo. Muda wa mjadala hutofautiana kulingana na swali na jinsi mjadala unavyokwenda. Katika hatua ya mwisho, mwalimu huchagua wanafunzi wachache kushirikishana darasa mawazo yao. Mbinu hii ni nzuri kwa kuibua mijadala madarasani na kushirikishana maoni na mawazo.

#### **Mbinu #48 Kazi za Wawili Wawili

Walimu wanaweza kupanga wanafunzi wawili wawili kushirikiana katika somo lolote. Hii huwapa wanafunzi fursa ya kujifunza kwa wenzao na kuzungumzia kile wanachojifunza. Ifuatayo ni baadhi ya mifano.

**Kuandika:** Wanafunzi wanaweza kutafakari au kujadili na wenzao mawazo yaokabla ya kuanza zoezi la kuandika darasani. Vile vile, wanaweza kutoa maoni yao kuhusu uandishi wa wenzao mwishoni mwa kipindi. Pia, wanafunzi wanaweza kusoma kazi zao kwa wenzao wanaoweza kuwapa mrejesho na maoni. Mwalimu anaweza pia kutoa mazoezi na kuwapanga wawili wawili ili waandike kitu fulani pamoja, hasa kwa muda wa mazoezi ya kuelekezwa. Baadaye, wanafunzi wanaweza kupitia na kurekebisha kazi za wenzao ili kusahihisha makosa na kutoa mrejesho wa zoezi hilo la kuandika.

**Kusoma:** Usomaji rika ni njia nzuri sana ya kuwasaidia wanafunzi kuboresha usomaji wao. Wanafunzi huwasomea wenzao. Wanapokezana kuwa "mwalimu" na "msomaji". "Mwalimu" humsaidia "mwanafunzi" wake kutamka maneno na huuliza maswali ya ufahamu yaliyoandaliwa na mwalimu mwenyewe. Baadaye wanapokezana nafasi zao. Usomaji huu vile vile huwasaidia wanafunzi kuboresha usomaji kwa ufasaha – sauti inavyopanda na kushuka, kasi na wepesi katika usomaji, na kupanga makundi ya maneno pamoja ili kuunda virai vyenye maana.

**Hisabati:** Vipindi vya hisabati, hufanya kazi pamoja kutatua maswali, kukagua kazi za wenzao, na kuelezea mawazo yao kwa kutumia misamiatihusika.

**Masomo mengine:** Wanafunzi wanaweza kufanya kazi za wawili wawili katika somo lolote, hasa kwa muda wa mazoezi au wa kukazia maarifa. Hao wawili wawili huongozana kujifunza. Wanajibu maswali pamoja, na kujadili wakiwa wanafanya kazi. Wanaweza kupokezana kujibu au wanaweza kufanya kazi hiyo pamoja. Ni vyema mwalimu akitoa mwongozo ili wanafunzi waelewe jinsi ya kufanya kazi pamoja na wanachotakiwa kukifanya kwa wakati huo wa zoezi.

****Mbinu #49 Ufundishaji Rika**

Ufundishaji rika ni mbinu nzuri sana kwa kuwasaidia wanafunzi wenye ugumu. Katika mbinu hii, mwanafunzi bora "humfundisha" mwanafunzi mwenye ugumu. Mfano, kwenye kusoma, msomaji mzuri hupangwa na yule mwenye ugumu katika kusoma habari au kitabu. Mfundishaji rika hufuatilia na kumsaidia mwenzake kutamka maneno, kutafuta maana na kuuliza maswali ya ufahamu. Hawa wafundishaji rika pia wanaweza kupewa kazi za vikundi. Wanafunzi ambao wameelewa ujuzi au mada wanaweza kusaidia katika kuongoza mijadala ya vikundi, kuwasilisha taarifa, kujibu maswali, na kuwasaidia wenzao kutafuta majibu ya maswali. Wakati mwingine wanafunzi huelewa vizuri wanapoelezewa na wenzao kuhusu dhana Fulani kuliko wanavyoelezewa na mtaalamu.

### 7.2 Kazi za Vikundi

Walimu wanaotumia *LCT* hutoa fursa za maana kwa wanafunzi kufanya kazi za vikundi. Kufanya kazi katika vikundi kwa ufanisi ni jambo la muhimu shuleni na katika maisha. Kuna maarifa muhimu, mitazamo, na mazoea yanayofanya vikundi kufanya kazi kwa makini shuleni, katika maeneo ya kazi, au katika maswala ya kijamii na maisha ya familia. Wanafunzi wanaojifunza kushirikiana vizuri na wenzao pia huwa wanaandaliwa kushirikiana vizuri mara baada ya maisha ya shule. Kazi za vikundi ni kifaa muhimu kwa walimu katika kuelekeza ufundishaji wao kwa wanafunzi walio na mahitaji yanayofanana ya ujifunzaji na kwa walimu kuwasaidia wanafunzi katika vikundi vidogo kuliko darasa zima.

Nchini Tanzania, *kazi za vikundi* hutumika zaidi katika *LCTs* (pamoja na *maswali na majibu*). Hata hivyo, utafiti uliofanywa madarasani na wahadhiri wa Chuo Kikuu Cha Kikatoliki cha Mwenge ulionyesha kuwa walimu ambao hawajaajiriwa na walioajiriwa mara nyingi hawana maarifa ya kuwezesha kazi za vikundi kwa ujifunzaji makini. Sehemu hii inatoa miongozo (si mbinu) ya kazi za vikundi zinavyoweza kuendeshwa kwa ajili ya ujifunzaji makini.

### 7.3 Weka Matarajio ya Kazi za Vikundi

Mikutano ya vikundi yenye ufanisi huundwa kutokana na tabia makini na matarajio ya kikundi. Walimu wazuri hufundisha, kurekebisha na kufanya mikutano yenye matarajio. Matarajio yanaweza kutofautiana lakini ifuatayo ni baadhi ya mifano: mtu anapoongea, wengine wanaweza kukubaliana kupinga, thamini au kubali kwamba watu wana mitazamo tofauti tofauti, kila mmoja anashiriki, wanafunzi hupokezana, wanafunzi hunyosha mikono kabla ya kuongea, makubaliano yanafanyika kwa kura au kwa mapatano, watu wapewe majukumu, na kadhalika. Walimu wanatakiwa kufikiri ni tabia zipi za mkutano ambazo watu wanataka kuziimarisha na kuhakikisha kuwa wanaboresha maarifa yao. Na pia wanatakiwa kutoa

maelekezo yanayoeleweka juu ya namna kila mwanafunzi na timu nzima watakavyopewa alama. Mara nyingi hii hufanyika kwa kutumia mwongozo unaoonyesha mgawanyo wa alama.

**7.4 Uundaji wa Vikundi vyenye Ufanisi**

Walimu wana njia tofauti tofauti za kuunda vikundi kwa kuchagua kuanzia muda wa kuandaa na kuwasilisha somo.

*Kwa usimamizi wa mwalimu au mwanafunzi*: Maamuzi ya kwanza ni kama kikundi kitasimamiwa na mwalimu au mwanafunzi. Kikundi kinachoongozwa na mwalimu huleta ufanisi endapo ni kikundi kidogo na cha wanafunzi wanaohitaji maelekezo ya pekee ambayo ni mwalimu tu anayeweza kuyatoa. Mwalimu huongoza michezo ya kurudia, pale wanafunzi wanapotakiwa kujibu maswali wanapokuwa kwenye kikundi, pia huchekesha na huwa makini. Vikundi vinavyoongozwa na wanafunzi huendeshwa ili kutumia maarifa ambayo yameshafundishwa, kujadili maswali ya malengo ya ujifunzaji, kuzungumzia kuhusiana na vitabu walivyoshirikishana, kumalizia kazi mradi na kujifunza kuwa makini katika kazi za vikundi. Mikutano ya vilabu vya vitabu ni mfano wa mijadala inayoongozwa na wanafunzi ambapo kila mwanafunzi anasoma kitabu hicho hicho, kuibua maswali ya mjadala na kukutana na klabu nyingine ili kujadili maswali hayo.

*Kikundi chenye uwezo sawa au uwezo mseto:* Jambo lingine la kufikiria ni uwezo sawa wa wanakikundi au uwezo mseto ambapo wenye uwezo mkubwa na uwezo mdogo wote wapo kwenye kikundi kimoja. Katika madarasa ya usomaji wa awali, vikundi vya kusoma hupangwa kulingana na uwezo. Hii humsaidia mwalimu kutoa maelekezo kwa wanafunzi wenye mahitaji sawa ya ujifunzaji. Kikundi cha wanafunzi wenye uwezo tofauti tofauti hufanya vizuri pale lengo linapokuwa ni kuhamasisha mjadala kupitia uwezo wao na kutoa fursa kwa wale wenye uwezo mkubwa kuwasaidia wenzao katika kikundi. Vikundi vya aina hii vina nguvu katika mijadala ya masomo ya kijamii, mijadala ya klabu za uandishi ambazo wanafunzi wanashirikishana na kukosoana katika uandishi wa kila mmoja wao, na kumfanya mwalimu mwongozaji wa timu katika michezo ya kurudia maarifa.

*Vikundi vinavyoweza kubadilikabadilika:* Vikundi huwa na uwezo wa kubadilikabadilika kutegemeana na wahusika. Wanafunzi huondolewa kwenye kikundi kutegemeana na mahitaji. Vikundi hivi vinaweza kubadilika siku kwa siku, wiki kwa wiki, au kila mwezi. Vikundi vinavyobadilika huwa vinafanya kazi muda wa mazoezi ya mmoja mmoja kwa wanafunzi ambao hawajamudu vizuri ustadi wa kufanya kazi pekee yao. Kwa mfano, katika hisabati, wanafunzi ambao hawajafahamu vizuri maarifa ya kila siku huwekwa katika vikundi vidogo vidogo ili kufanya kazi na mwalimu kwa muda huo wa kipindi.

**7.5 Kutumia Mwongozo Unaoonyesha Mgawanyo Wa Alama kwa Kazi za Vikundi**

Walimu wazuri siku zote hutumia mwongozo wa mgawanyo wa alama [*Rubrics*] kupima kazi za vikundi. Mwongozo huu huelezea namna kazi mradi au kazi zozote zitakavyopangiwa alama. Mwongozo huu una sehemu muhimu za ujuzi ambazo hupimwa na kupangiwa alama na kisha huunganishwa kutoa alama ya jumla kwa kazi mradi. Mwongozo huu husaidia wanafunzi kuona matarajio halisi kwa kazi mradi na jinsi watakavyopata alama kama mtu binafsi au kama kikosi. Kazi mradi yoyote ya kikundi makini lazima ianze na mwisho huu akilini -ni nini malengo ya ujifunzaji na yanaakisiwa vipi katika mwongozo wa mgawanyo wa alama ili wanafunzi wawe na lengo ambalo ni dhahiri mbele yao.

****Mbinu #50 Vikundi vya Mjadala Vinavyoongozwa na Wanafunzi**

Kwa kutegemea ukubwa wa darasa, mwalimu anaweza kuchagua kutumia vikundi vikubwa au vidogo. Mara tu darasa linapogawanyika kwenye vikundi, wanafunzi hujadili mada waliyopewa na mwalimu. Vikundi hivi ni fursa ya wanafunzi kushirikishana mawazo na kutatua matatizo na wenzao. Mwalimu anapaswa kuelezea matarajio na tabia zinazotakiwa kwenye vikundi. Kazi ya vikundi inapokuwa ikiendelea, mwalimu huzungukia vikundi vyote darasani, huwasikiliza wanakikundi na kutoa maoni,

mawazo na masahihisho endapo kikundi kimepoteza mwelekeo au kama kuna mjadala kuhusu taarifa isiyo sahihi. Mwisho wa mjadala, kikundi kimoja au viwili hushirikisha darasa zima. Kisha mwalimu anaweza kusaidia kufafanua, kufupisha na kulielekeza darasa kwenye lengo la kujifunza na mawazo makuu ya somo.

****Mbinu #51 Uwasilishaji wa Mada Darasani**

Hii hufanywa kupitia kwa kazi za vikundi. Mwalimu huigawanya mada – mfano wahusika kwenye riwaya za kidato cha tatu somo la Kiingereza - katika vipengele vidogo vidogo (kama wahusika wa *Things Fall Apart*). Wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo huandaa kipengele kimojawapo watakachojadili na kuwasilisha mbele ya darasa kwa muda wa dakika 5 mpaka 10. Kwa mfano huu, mwalimu anaweza kuomba kikundi kimoja wajadili wasifu wa Okonkwo na kingine kiwasilishe Nwoye. Mwalimu huwapa wanafunzi muda wa kutosha wa kujiandaa. Baada ya mjadala, wanapewa muda wa kuwasilisha mada yao darasani pamoja na kujibu maswali yatakayoulizwa na mwalimu au wanafunzi wengine. Baada ya kila kikundi kuwasilisha mada yao mwalimu husahihisha makosa yaliyojitokeza katika uwasilishaji na kuwauliza wanafunzi maswali yanayochochea matumizi ya nyanja za juu za utambuzi kama kulinganisha na kutofautisha wasifu wa Okonkwo na Nwoye baada ya kuwasilisha mjadala. Njia hii ni nzuri na inafaa sana kwa wanafunzi wa kidato cha 3 na cha nne ambao uwezo wao wa lugha ni mkubwa, japo hata wa kidato cha kwanza na cha pli wanaweza kuandaa kazi fupi za kuwasilisha mbele ya darasa kama njia ya kujenga uelewa wao kuhusu mada Fulani na stadi ya kuzungumza.

**Mbinu #52 Usomaji wa Awali Unaofuatiwa na Mijadala ya Vikundi**

Mbinu nyingine ni kuwapa wanafunzi kazi ya kufanya nyumbani, kusoma na kujibu maswali kuhusiana na mada itakayojadiliwa darasani siku ifuatayo. Wanafunzi wanaporudi darasani, mwalimu huwaomba kukaa katika vikundi ili kujibu na kujadili maswali kuhusiana na walichokisoma nyumbani. Kwa kuwa wanafunzi wanakuwa walishasoma, inakuwa rahisi kwao kujadiliana na kubadilishana uelewa, na hii husababisha matumizi mazuri ya muda wa vipindi. Wanafunzi wanapojadili, mwalimu huwazungukia ili kuwasaidia sehemu ngumu zinazowasumbua. Kisha wanafunzi huwasilisha mawazo yao na mwalimu hufanya usahihishajis wa makosa yao na kufupisha mawazo makuu ya somo.

**Mbinu #53 Maigizo**

Njia hii ni sawa na ya mjadala kwenye vikundi lakini hii huhusisha nyanja za juu za utambuzi wa matumizi na uchambuzi kwa kutumia vipengele na taratibu muhimu ambazo mwalimu amezilenga katika maisha halisi, matukio ya siku kwa siku. Mwalimu huwapanga wanafunzi katika vikundi, kisha huwapatia kadi zilizoandikwa mambo yanayohusu maisha halisi. Kila kadi huwa na taarifa au majukumu yanayohusiana na mada. Wanafunzi huchukua majukumu waliyoagizwa kama yalivyojieleza katika kadi hizo. Baada ya hapo hutumia dakika chache kuelewa majukumu yao vizuri. Muda ukifika, kila mwanakikundi huigiza sehemu yake bila kusoma. Kila jukumu litawakilisha sehemu fulani ya kipengele muhimu. Mwisho wa igizo, mwalimu huwauliza wanafunzi maswali ili kupima uelewa juu ya vipengele na mawazo makuu yaliyowasilishwa. Kwa mfano, mwalimu wa uraia akiwa amekusudia kufundisha kipengele cha unyanyasaji wa kijinsia, anaweza kuandaa kadi kutokana na mifano iliyopo kwenye magazeti au katika jamii za kitanzania za leo ambapo kuna mitazamo tofauti tofauti kuhusiana na njia za kutatua unyanyasaji wa kijinsia, na nani ahusike na utatuzi huo.

**Mbinu #54 Kuwatoa Wanafunzi Nje ya Darasa**

Wanafunzi hutoka nje ya darasa katika vikundi, mfano mbele ya shule ambapo kuna nafasi kubwa. Hii inasaidia pale ambapo wanafunzi watakuwa wanaongea kwa sauti, kitu ambacho kingeleta shida kwenye darasa dogo. Mwalimu anaweza kuwaelekeza wanafunzi wakae chini, kila kikundi kivyake, ili awe anawazungukia kuwasaidia wanapopata ugumu. Mkakati huu hutumika kwenye shule zenye mikondo

mingi na walimu wachache wa somo husika. Ndani au nje ya darasa, wanafunzi huhamasishwa kujifunza wao kwa wao. Kutoka nje katika vikundi pia ni njia nzuri ya kutumia mazingira, kwa mfano kwenye somo linalohusu wadudu au mimea ambapo wanafunzi wanaweza kuvipata na kuvitambua.

**Mbinu #55 Makundi ya Chemshabongo**

Mbinu hii inafaa sana pale ambapo mwalimu amekusudia kufundisha vipengele vingi vya mada mpya ambavyo vinaeleweka kwa urahisi. Wanafunzi katika vikundi tofauti hupewa dhana za kusoma na kujadili , lakini kila kikundi hupewa taarifa tofauti na vingine. Ndipo mwalimu huvivunja vile vikundi na kuunda vingine vipya vikiwa na wahisika wa vikundi mbali mbali. Kila mwanakikundi huwafundisha wengine dhana zilizojadiliwa na kikundi chake cha awali ili kwa pamoja, wanafunzi wapate maarifa yote yaliyokusudiwa.

## SURA YA NANE

## LCTS KWA UPIMAJI NA HITIMISHO

Walimu wanaotumia *LCT* hutumia mazoezi ya wiki, majaribio ya kila mada na mazoezi ya kila siku kupima uelewa wa wanafunzi, ili kuwatambua wanafunzi wanaohitaji msaada na kuandaa kipindi kijacho. Vile vile, wakati wa kuhitimisha kipindi (mara nyingi dakika 5 za mwisho), mwalimu huwataka wanafunzi watafakari walichojifunza kwa kushirikishana kwa mjadala wa darasa zima, kujadili wawili wawili au kimakundi, kuandika majibu mafupi kwa maswali na kujaza tiketi za kutokea [*exit slips*]. Hatua hii ni muhimu kwa kumfanya mwanafunzi afikirie tena malengo ya ujifunzaji wa kila siku na walimu kupima uelewa wa wanafunzi.

### **Mbinu #56 Tiketi ya Kutokea

Tiketi ya kutokea ni kipimo kisicho rasmi na cha haraka ambacho mwanafunzi hujaza mwishoni mwa kipindi. Mwalimu hutoa tatizo au swali kwa wanafunzi ambalo wanatakiwa kulitatua au kulijibu. Mwalimu hukusanya majibu ya wanafunzi pale wanafunzi wanapoondoka ili aweze kupima uelewa wa wanafunzi. Njia hii hutumika kwa ajili ya kuandaa somo lijalo na kwa kutambua wanafunzi wanaohitaji msaada zaidi. Tiketi za kutokea mara nyingi huandikwa kwenye karatasi au daftari ndogo za kumbukumbu au kwenye vibao vidogo vya kila mwanafunzi vinavyoweza kushikiliwa hewani.

### **Mbinu #57 Nionyeshe

Katika mbinu hii wanafunzi huonyesha kazi zao kwa mwalimu ambaye anazunguka darasani kwa haraka kupima ujifunzaji wa wanafunzi. Swali hutolewa kwa wanafunzi ili walitatue au kulijibu. Wanafunzi huonyesha majibu yao kwa kuandika kwenye vibao vidogo, vijidaftari vidodo au mikononi mwao. Ukisema au kutoa ishara ya "nionyeshe", wanafunzi huonyesha kazi zao. Njia hii ni sawa na kutoa tiketi ya kutokea lakini hufanywa kwa pamoja ambapo wanafunzi wote huonyesha kazi zao kwa pamoja. Kisha mwalimu huangaza darasani kuona kama wanafunzi wameelewa kipengele hicho au kama wamepata maarifa. Walimu wanaweza kupima kwa haraka ni nani ameelewa na ni nani anahitaji msaada zaidi.

### ** Mbinu #58 Vichwa Chini, Mikono Juu

Pale mwalimu anapofikiri wanafunzi wanaweza kufedheheka au kutoridhika kuonyesha kuwa hawaelewi kitu, wanafunzi wanaweza kuambiwa wainamishe vichwa vyao kwenye dawati, wafumbe macho, na wajibu maswali ya ufahamu yatakayoulizwa na mwalimu kwa kunyosha mikono yao juu kama wanafikiri jibu ni ndio au hapana, A au B, 1 au 2, na kadhalika. Mwalimu anaweza kuwahakikishia wanafunzi kuwa hilo si jaribio ila anataka kujua kama wameelewa kabla hawajaenda kwenye mada nyingine au kama msaada zaidi unahitajika kwenye kipengele hicho. Baada ya kila swali, mwalimu anaweza kuandika idadi ya wanafunzi waliojibu swali kwa usahihi na kukadiria kama ni 20, 30, 40 au 80% walio sahihi. Nchini Tanzania, upimaji huu unafaa sana kwa kupata taarifa zinazotakiwa kujaza sehemu ya *tathmini ya wanafunzi* katika andalio la somo.

### Mbinu #59 Mchezo wa Kurusha Mpira

Hii ni nusu - marudio na nusu-changamsha unapotaka kumaliza kazi inayohitaji ufuatiliaji wa hali ya juu. Kila mtu asimame na kufanya mfano wa duara. Si lazima iwe kamilifu, lakini wote wageukie ndani na kutazamana. Kisha mwalimu anauliza swali. Mfano wa kemia somo la mfumo radidia, mwalimu atauliza, "Ni elementi zipi zinazopatikana kwenye mfumo radidia?" Akishauliza, anamrushia mwanafunzi mmoja mpira wa tenisi au wa karatasi na kumtaka ataje elementi moja. Akishajibu, anamrushia mwingine atakayetaja elementi ya pili, na kadhalika. Mbinu hii inaweza pia kutumika kwa kuwafanya wanafunzi kutoa maoni yao mwishoni mwa somo, mathalan kwa kuwauliza mambo waliyoyaona kuwa ya msingi zaidi katika mada husika. Mwalimu huuliza swali, humrushia mwanafunzi mmoja mpira ili atoe maoni yake, kisha humrushia mwingine naye atoe maoni yake, na kadhalika.

**Mbinu #60 Mchezo wa Kofia**

Waombe wanafunzi wakae kwenye vikundi na waandike maswali, yanayohusiana na mada iliyojadiliwa, kwenye vipande vya karatasi darasani. Kila kikundi kinatakiwa kuandika majibu mafupi mafupi moja au mawili na kuweka karatasi hizo za majibu ndani ya 'kofia' mbele ya darasa. Chagua wanafunzi wachache (mf. 6) hapa na pale kwa kutumia orodha ya wanafunzi darasani. Chukua swali moja kutoka ndani ya kofia na uwaambie wanafunzi hao walijibu. Yeyote anayejua jibu kati ya hao sita anaweza kujibu. Kikundi kinapata alama za ushindi ikiwa miongoni mwa wale sita hayupo anayeweza kujibu swali lao.

**Mbinu #61 Kipande cha Mfano**

Mbinu hii ni sawa na mwito wa baridi, isipokuwa hii inalenga uandishi. Baada ya kuandika, mwalimu huchagua mwanafunzi asome insha, shairi, au chochote alichokiandika mbele ya darasa. Darasa hutoa mrejesho chanya na kisha hujadili namna uandishi huo unavyoweza kuboreshwa. Mbinu hii huhamasisha wanafunzi kuboresha uandishi wao, hupongeza kazi za wanafunzi, na husaidia wanafunzi wote kuboresha uandishi wao bila kujali viwango vyao vya uandishi.

**Mbinu #62 Kiti cha Moto**

Chagua mwanafunzi mmoja au wanafunzi kadhaa waende mbele ya darasa na wakae chini mahali palipoandaliwa. Mwanafunzi yeyote anaweza kuwauliza swali wanafunzi hao kuhusiana na zoezi lililotolewa, jaribio, au kipengele chochote cha somo na wanafunzi walioko kwenye kiti cha moto wanapata alama za vema kwa swali lolote watakaloweza kujibu vyema.

**Mbinu #63 Toa Muhtasari**

Hii ni aina ya tiketi ya kutokea ambapo wanafunzi huandika muhtasari wa walichojifunza somo linapokuwa linahitimishwa. Wanaandika jibu linalohusu lengo la somo au kutoa muhtasari wa somo zima wawili wawili au katika vikundi vidogo. Wanafunzi wanapokuwa wanaandaa muhtasari wa somo, mwalimu huzunguka ili kuwasikiliza na kupima uelewa wao.

**Mbinu #64 Kusahihisha kwa Mnyororo**

Wanafunzi wanaweza kusahihishana kazi zao. Njia moja inaitwa "Kusahihisha kwa Mnyororo" [*Chain Checking*]. Mwanafunzi wa kwanza anapomaliza kazi yake humpelekea mwalimu. Mwalimu huisahihisha kazi hiyo kwa kukagua makosa na kisha mwanafunzi huyo huwa msahihishaji. Wanafunzi wengine wakimaliza kazi zao na kusahihishwa, nao huwa wasahihishaji wa wenzao. Ikiwa mwanafunzi atakosa swali, msahihishaji atalizungushia duara na mwanafunzi huyo ataenda kwa mwalimu au kwa mwanafunzi mwezeshaji kupata msaada zaidi. Njia hii inaweza kutumika kukagua kwa haraka na kumfanya mwalimu kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji msaada. Wanafunzi hupata majibu ya mazoezi yao papo kwa hapo na mwalimu anaweza kuelekeza nguvu kwa wanafunzi wanaohangaika.

## SURA YA KUMI

## USIMAMIZI WA DARASA

Walimu wanaotumia *LCT* ni lazima wawe wasimamizi wazuri wa darasa. Huwafundisha wanafunzi wao kuhama kutoka kazi moja kwenda kazi nyingine haraka, kwa urahisi na kwa utaratibu. Hufundisha, hutumia na kusimamia utaratibu wa kila siku ili mwanafunzi ajue nini cha kufanya siku nzima. Hawa husimamia kwa ustadi wa hali ya juu taratibu za darasani.

### **Mbinu #65 Weka Taratibu

Hakuna kitu kizuri mnapoanza mwaka wa masomo kama kuundaa taratibu na mtiririko mzima wa kazi za kila siku kama vile namna ya kuingia na kutoka darasani, namna ya kukaa mstarini, namna ya kuomba ruhusa ya kuenda msaalani, namna ya kunyosha mikono ili uongee, namna ya kufanya kazi na wanafunzi wenzao, namna ya kufanya mazoezi katika vikundi, namna ya kufanya kazi kimya kimya na utaratibu wa shughuli zote za siku darasani. Kuweka taratibu hizi za kila siku na kuzifanyia kazi hutengeneza mazingira salama na yenye mpangilio mzuri wa ujifunzaji. Taratibu hizi ni lazima zifuatwe mwaka mzima ili kulinda hadhi ya utendaji.

### **Mbinu #66 Matokeo – Ya Haki, ya Kueleweka na Thabiti

Pale mwanafunzi anapovunja sheria, walimu huwa na chaguo nyingi. Nimtume mwanafunzi ofisini kwa mkuu wa shule au kwa mkuu wa nidhamu? Nimuadhibu hapa hapa darasani? Niwasiliana na mzazi wake? Na kwa makosa yasiyo makubwa sana ni vizuri mwanafunzi akaadhibiwa palepale ili ajifunze kutokana na makosa, waadhibiwe na kurudi darasani waendelee na kipindi ili wasipoteze muda wa kipindi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kusema, “Amina, acha kuzungumza na Rose.” Matokeo ya adhabu yanatakiwa kuwa ya kueleweka na kuongezeka uzito. Hii ni kusema, mkosaji aanzie adhabu ndogo na hatua za kinidhamu ziendelee kuwa kali kama makosa yatarudiwa. Endapo Amina ataendelea kuzungumza na Rose, mwalimu anaweza kumwambia ahame kiti akakae karibu na Felix. Walimu pia wanatakiwa kuwa na usawa katika adhabu na kuhakikisha inaendana na kosa. Wanafunzi waadhibiwe kwa usawa ili kwamba mwanafunzi yeyote, na si Amina tu, akumbuke kwamba hairuhusiwi kuzungumza ovyo muda wa kipindi. Mwisho, walimu wapime ufanisi wa kuwaadhibu wanafunzi hadharani dhidi ya kuzungumza nao kwa faragha. Unapomuadhibu mwanafunzi mbele ya darasa, mwalimu anayemzingatia mwanafunzi anatakiwa kuifanya imara sauti yake na kujitawala kisaikolojia na baada ya kumaliza, aendelee na somo kama vile hakuna kitu kilichotokea. Hii huwafanya wanafunzi wajue kuwa ujifunzaji ni muhimu na ufundishaji na ujifunzaji utaendelea kama kawaida.

### **Mbinu #67 Ishara za Kimya

Katika madarasa changamfu, wanafunzi huongea wawili wawili au na wanafunzi wengine katika hatua tofauti tofauti za kipindi. Hivyo basi, inashauriwa mwalimu kutumia ishara za kimya kuwatuliza wanafunzi darasani. Kuna ishara nyingi za kuwatuliza wanafunzi darasani kama vile kuimba [*chants*], kupiga makofi kwa utaratibu na wanafunzi kurudia, kuwanyamazisha wanafunzi kwa kuwaamrisha wasikilize, na mbinu zingine. Ifuatayo ni mifano ya ishara za kimya/kuwanyamazisha wanafunzi.

> *“Kama Unanisikia Piga Makofi Mara Moja”*
>
> Mwalimu husema kwa sauti ya kawaida au taratibu, “Kama unanisikia piga makofi mara moja,” kisha husikiliza kama wanapiga makofi mara moja na kwa pamoja. Kama wanaendelea kuongea, mwalimu huwaambia “piga makofi mara mbili” na kisha husubiri wawe kimya. Kama mwanafunzi bado anaongea, mwalimu anaweza kusema, ”Ninasikia mwanafunzi bado anaongea” na kisha husubiri kuona kama kuna kimya. Ikilazimu, mwanafunzi anayeendelea kuongea ahutambuliwa na kuambiwa kwa jina lake awe kimya. Kuacha na kusubiria katika upigaji makofi

husababisha wanafunzi kusikia darasa likiwa kimya na huhamasiha wanafunzi wengine wanaoendelea kuongea kuwa kimya.

*Makofi, Makofi, Makofi*

Mbinu hii ya kunyamazisha wanafunzi huanza na mwalimu kupiga makofi na kisha hufuatwa na wanafunzi. Mwalimu anapoacha kupiga makofi, wanafunzi nao wanatakiwa kuacha na wawe kimya. Kisha mwalimu anaweza kusubiria kusikia kelele tena na anaweza kuanzisha tena upigaji makofi kama ikibidi.

*3, 2, 1*

Mwalimu huinua mkono na kunyosha vidole vyake vitano. Taratibu anasema “Tano”, na kushusha kidole kimoja, halafu anasema “Nne”, na kushusha kidole kingine na kusema “Tatu,” na kadhalika. Anapokuwa amebakiza kidole kimoja tu hewani na kusema “Moja,” wanafunzi wanatakiwa kuwa kimya.

*Nipe Tano*

Mwalimu huweka mkono wake hewani na kusema “Nipe tano”. Kisha husubiria wanafunzi wote waweke mikono hewani wakisubiria maagizo.

*Darasa, Darasa, Darasa … Ndio, Ndio, Ndio*

Mwalimu anaweza kusema “darasa, darasa, darasa” kwa sauti yoyote-sauti ya kawaida, sauti ya kuchekesha, sauti ya mnong’ono, au sauti nyingine yoyote na wanafunzi huitikia kwa pamoja “ndio, ndio, ndio,” kwa kuiga sauti alioitumia mwalimu. Wanafunzi wanapomaliza kusema “ndio” wanakuwa kimya.

****Mbinu #68 Kila Mtu Anafanya Hivyo**

Mbinu ya “kila mtu anafanya hivyo” ni njia muhimu ya kuweka viwango vya juu na matarajio makubwa darasani. Hivyo, anapotoa ishara ya kimya, mwalimu husubiri mpaka mwanafunzi wa mwisho aache kuongea. Mwalimu anaweza kusema “Ninatafuta 100%” au “hii ni kama 100%” kuwafanya wanafunzi wajue kwamba hata kwenye darasa lenye wanafunzi wengi, kila mwanafunzi anatakiwa kuwajibika. Ni sawa na taratibu na maelekezo mengine. Walimu wa *LCT* huweka matarajio ya juu kwa 100% ya wanafunzi wao. Hakuna kumradhi. Hakuna walakini. Wanasema hivyo kwa sauti imara na yenye mwamko. Wanajizuia kuwakaripia wanafunzi na badala yake wanafikisha ujumbe unaoeleweka kwa wanafunzi kuwa hivi ndivyo tunavyofanya tukiwa darasani.

****Mbinu #69 Sauti Imara na Msimamo**

Walimu wanaotumia *LCT* hutumia sauti yenye nguvu na uimara wanapowaonya wanafunzi na kuwaelekeza. Pia husimama na kumwangalia mwanafunzi anayetenda vibaya hasa wanaposhughulikia tatizo sugu la tabia mbaya. Ni muhimu kwa walimu kujitawala kisaikolojia kadiri wawezavyo na kufikisha ujumbe kwa uimara kwamba utovu wa nidhamu hauruhusiwi darasani humu.

****Mbinu #70 3/ 5/ 1**

Mkakati huu hutumika muda wa mazoezi ya mmoja mmoja na mwalimu huzunguka darasani kuimarisha vipengele vya somo na kusimamia kazi za wanafunzi. Mwalimu huanza kwa dakika tatu kuwaelezea wanafunzi nini cha kufanya katika kazi yao. Pale tu mwalimu atakapoona wanafunzi wameanza kufanya kazi waliyoagizwa, atazungukia darasa kuwasaidia. Hivyo, mwalimu huwasaidia wanafunzi kwa takriban dakika tano. Baada ya hapo mwalimu husimama na kuwasaidia wanafunzi wote kama kwa dakika moja

hivi kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anahusika katika kazi. Na kisha mwalimu humsaidia mwanafunzi kwa takribani dakika tano na tena kwa dakika moja huwasaidia wanafunzi wote na kutoa mapendekezo kwenye dhana zilizokosewa katika makundi. Hili hurudiwa karibia kipindi kizima cha kujisomea. Njia hii imeandaliwa kuwasaidia walimu kufanya uwiano kati ya msaada kwa mwanafunzi mmoja mmoja na msaada kwa darasa zima. Kama mwalimu atatumia muda mwingi kumsaidia mwanafunzi mmoja au wawili nayo inaweza kuleta shida.

## HITIMISHO

Walimu wanaotumia mbinu za *LCT* wana mawazo na ustadi wa kuwasaidia wanafunzi kujifunza na kufanikiwa. LCTs katika kiongozi hiki zimethibitishwa kuwa na ufanisi duniani kote. Ni matumaini yetu kwamba wewe, kama mwalimu kwa taaluma, utajaribu baadhi ya mbinu hizi na kuendelea kuboresha ustadi wako katika ufundishaji. Tnafahamu kwamba kuna mbinu zingine nyingi na nzuri ambazo hazikuandikwa katika kiongozi hiki. Baadhi ya mbinu hizo zinaweza kuongezwa kwenye matoleo ya usoni ya kiongozi hiki. Tunapendekeza ujaribu mbinu moja kwa wakati na kisha kutafakari ni mbinu ipi iliyoleta mafanikio na ni ipi haikuzaa matunda katika somo. Ni mchakato wa kujaribu mbinu mpya, kuzirudia, na kubuni kifaa kipya chenye ufanisi unaomfanya mwalimu kuwa yule anayemzingatia mwanafunzi. Tunatumaini kwamba kiongozi hiki kitaleta ari na kutoa mawazo halisi kwa walimu ambao wanataka kuleta mabadiliko katika maisha ya wanafunzi wao.

## TASNIFU


Freire, P. (2000). *Pedagogy of the Oppressed*. New York: Bloomsbury.

Christodoulou, J. A. (2009). Updates to the Theory of Multiple Intelligences: What Matters for Schools. *The School Administrator* 66(2), 22-26.

Hein, E. G. (1991). *Constructivist Learning Theory*. A paper presented at CECA (International Committee of Museum Educators) Conference Jerusalem Israel, 15-22 October 1991.

Lemov, L. (2010). *Teach like a champion*. San Fransisco: Jossey-Bass.

United Republic of Tanzania (1999). *Development Vision2025*. Available at http://www.tanzania.go.tz/vision.htm.

Vavrus, F. (2011). *Faculty-to-Faculty Training Guide*. Moshi: TIA Unit – Mwenge Catholic University.

Vavrus, F. (2014). *TIA Workshop Module*. A. Rugambwa, and Bahiya, A. (Eds). Moshi: TIA Unit – Mwenge Catholic University.

Vavrus, F., & Bartlett, L. (Eds) (2013). *Teaching in Tension: International Pedagogies, National Policies, and Teachers' Practices in Tanzania*. Rotterdam, Netherlands: Sense Publishers.


### WEBSITES


http://www.teindia.nic.in/files/teacher_trg_module/17_cambodia%20module.pdf

http://www.training-games.com/pdf/40FreeIceBreakers.pdf

https://theonlinepd.wordpress.com/p-3-lesson-planning/creating-a-strong-hook/